# ULINZI KWA WAHANGA WA MIGOGORO YA KUTUMIA SILAHA KATIKA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU NA SHERIA YA KIISLAMU

(حماية ضحايا النزاعات المسلحلة في القانون الدولي الإنساني والشريعة الإسلامية)

**Mwandishi: Profesa Abdul-Ghaniy Abdul Hamid Mahmoud**

**Dibaji: Profesa Muhammad Sayyid At-Twantwawiy**
**Sheikh Mkuu wa Al-Azhar-Misri**

REFERENCE

COMITE INTERNATIONAL GENEVE
ICRC

International Committee of the Red Cross
Nairobi Regional Delegation,
Denis Pritt Road
P. O. Box 73226-00200 Nairobi, Kenya
T +254 20 272 3963
E-mail: nairobi@icrc.org

International Committee of the Red Cross
Hamza Aziz Street,
Plot No1736, Block B, Kahama Court-Masaki,
P.O. Box 23431 Dar es Salaam, Tanzania
T: (+255) 222 600 446/7/8/9
E-mail : daressalaam@icrc.org
www.icrc.org
© ICRC, December 2019

# ULINZI KWA WAHANGA WA MIGOGORO YA KUTUMIA SILAHA KATIKA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU NA SHERIA YA KIISLAMU

(حماية ضحايا النزاعات المسلحلة في القانون الدولي الإنساني والشريعة الإسلامية)

**Mwandishi: Abdul-Ghaniy Abdul Hamid Mahmoud**
**Mhadhiri wa Sheria ya Kimataifa**
**Chuo Kikuu Cha Al-Azhar**

**Dibaji: Profesa Muhammad Sayyid At-Twantwawiy**
**Sheikh Mkuu wa Al-Azhar-Misri**

**Kimesahihishwa na Sheikh Saidi Salim Saidi – Bawazir**

# YALIYOMO


| | |
|---|---|
| Haki Miliki | 3 |
| Yaliyomo | 5 |
| Dibaji | 8 |
| Utangulizi | 10 |
| **MLANGO WA KWANZA** | **17** |
| Ulinzi Kwa Wahanga wa Migogoro ya Kimataifa ya Kutumia Silaha | 17 |
| Sura ya Kwanza | 18 |
| Ulinzi kwa majeruhi, wagonjwa na waliokumbwa na maafa baharini, katika sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu na sheria ya Kiislamu | 18 |
| a) Tafiti ya kwanza | 19 |
| Ulinzi kwa majeruhi, wagonjwa na waliokumbwa na maafa baharini katika sheria ya kimataifa ya kibinadamu | 19 |
| b) Tafiti ya Pili | 22 |
| Ulinzi kwa majeruhi, wagonjwa na waliokumbwa na majanga baharini, katika Sheria ya Kiislamu. | 22 |
| c) Tafiti ya Tatu | 25 |
| Uwiano uliopo kati ya Sheria ya Kiislamu na Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu | 25 |
| Sura ya Pili | 26 |
| Ulinzi kwa mateka katika sheria ya kimataifa ya kibinadamu na sheria ya kiislamu | 26 |
| a) Tafiti ya Kwanza | 27 |
| Makusudio ya Mateka wa vita katika Sheria ya Kiislamu | 27 |
| b) Tafiti ya Pili | 31 |
| Ulinzi kwa mateka katika sheria ya kimataifa ya kibinadamu | 31 |
| c) Tafiti ya Tatu | 36 |
| d) Ulinzi kwa mateka katika sheria ya kiislamu | 36 |
| Sura ya Tatu | 43 |
| Ulinzi kwa watu waliopotea na maiti katika sheria ya kimataifa ya kibinadamu na sheria ya kiislamu | 43 |
| a) Tafiti ya Kwanza | 44 |
| Ulinzi kwa watu waliopotea na Maiti, katika Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu | 44 |

b) Tafiti ya Pili 46
Ulinzi kwa watu waliopotea na Maiti, katika Sheria ya Kiislamu 46
Sura ya Nne 50
Ulinzi kwa raia na vyanzo vya huduma za kijamii katika Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu na Sheria za kiislamu 50
a) Tafiti ya Kwanza 51
Ulinzi kwa raia, katika Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu na Sheria ya Kiislamu 51
Kifungu cha kwanza
Ulinzi kwa raia, katika Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu 51
Kifungu cha Pili 53
Ulinzi kwa raia katika Sheria ya Kiislamu 53
b) Tafiti ya Pili 57
Ulinzi kwa vyanzo vya huduma za kijamii, katika Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu na Sheria ya Kiislamu 57
Kwanza: Ulinzi kwa vyanzo vya huduma za kijamii, katika Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu 60

MLANGO WA PILI 63
Ulinzi kwa wahanga wa migogoro ya ndani ya kutumia silaha 63
Sura Ya Kwanza 65
Maana ya utekelezaji wa Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu katika migogoro ya ndani ya kutumia silaha na sehemu ya utekelezaji wake 65
Makusudio ya utekelezaji wa Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu katika migogoro ya ndani ya kutumia silaha katika Sheria ya Kiislamu 68
Sura ya Pili 71
Malengo ya Ulinzi ya kuwalinda wahanga wa migogoro ya ndani 71
a) Tafiti ya Kwanza 72
Ulinzi kwa wapiganaji 72
Kifungu cha kwanza 72
Ulinzi kwa mateka
1. Ulinzi kwa mateka katika Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu 72
2. Haki za mateka katika Sheria ya Kiislamu 73
Kifungu cha Pili 76
Ulinzi kwa majeruhi, wagonjwa na waliopata majanga baharini 76
1. Ulinzi kwa majeruhi, wagonjwa na waliopata majanga baharini, katika Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu 76
2. Ulinzi kwa majeruhi, wagonjwa na waliopatwa na majanga baharini katika sheria ya kiislamu 77

Kifungu cha Tatu 81
Kuwalinda maiti na watu waliokosekana 81
Tafiti ya Pili 85
Ulinzi kwa raia 85
1. Ulinzi kwa raia, katika Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu 85
2. Ulinzi kwa raia, katika Sheria ya Kiislamu 87
Mwisho wa Tafiti 88

## ULINZI KWA WAHANGA

# DIBAJI

### Bismillahil Rahmanil Rahim

Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu wote, na rehema na amani zimfikie Mjumbealiyetumwa kwa viumbe vyote, akiwa ni rehema kwa dunia nzima, Mtume Muhammad pamoja na familia na maswahaba wake.

Ama baada ya hayo yaliyotangulia,

Basi kwa hakika, Sheria ya Kiislamu ni sheria ya ulimwengu mzima ambayo inawataka binadamu wote kuitika wito wa tawheed (kuingia katika Uislamu), na inawalingania katika hilo kwa hekima na mawaidha yaliyo mazuri. Pia Sheria ya Kiislamu inajenga uhusiano mzuri kati ya waislamu na wasiokuwa waislamu, iwe ni wakati wa vita au amani. Kama ambavyo sheria hiyo, inaweka misingi madhubuti na ya lazima ambayo haifai kwenda kinyume nayo.

Na katika hili, Sheria ya Kiislamu ni ya kipekee, na tofauti kubwa iliyopo kati yake na sheria nyingine ni kwamba, kwenda kinyume na kanuni zake kunapelekea mtu kupata adhabu mara mbili, moja ni adhabu ya kesho akhera na nyingine ni ya hapa hapa duniani, na hii ndiyo sababu kubwa ya kuwa Uislamu unalinda haki za binadamu hata katika nyakati za vita, pasi na kuangalia kwamba binadamu hawa wawe ni wapiganaji au sio wapiganaji.
Ongezea kwamba, misingi ya Sheria ya Kiislamu inayowatetea wahanga wa vita, imejikita sana juu ya tabia nzuri na maadili ya kibinadamu. Na inajulikana kuwa, tabia nzuri ndio uzio wa mwenendo wa binadamu wa kuishi na wahanga wa vita, kwani Uislamu unawataka wafuasi wake wajitahidi sana kuishi vizuri na maadui zao pale tu wanapogeuka kuwa ni mateka na watakapokuwa hawana tena uwezo wa kupigana, kutokana na maradhi au majeraha. Pia Uislamu unakataza kuua au kumuadhibu majeruhi. Sambamba na hilo, aidha Uislamu unakataza kuua watu wasiopigana kama vile wanawake, watoto, wazee na wengineo ambao hawashiriki katika matendo ya kiadui dhidi ya waislamu.

Kuwaheshimu wahanga wa vita na kuishi nao vizuri, ni jambo linaloenda sawia kabisa na utukufu ambao Mwenyezi Mungu amempa mwanadamu, kwa kuwa mwanadamu ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu hapa ardhini. Ni vema kuashiria kwamba, Uislamu, kwa namna ulivyo, unalingania juu ya kuoneana hururma, kufanya uadilifu, upole na kumtendea wema mnyonge.

Kwa msingi huo, Sheria ya Kiislamu inahakikisha kwamba wahanga wa vita, vya ndani au vya kimataifa, wanapatiwa ulinzi na kuishi vizuri.Kuna ushahidi mwingi katika Qur'an na Hadithi za Mtume Muhammad (juu yake rehema na amani) kuhusu haki za binadamu na ulinzi waliopewa wahanga migogoro ya kutumia silaha, sawasawa wahanga hawa wawe ni mateka, majeruhi, wagonjwa au waliopotea na raia.

Kuhusiana na kuwatilia umuhimu raia, Uislamu umekataza kabisa kuharibu vyanzo vya huduma za kijamii ambazo ni hitajio la lazima kwa maisha ya binadanamu, kama vile kuharibu mimea, matunda, maji, mitambo ya umeme, mabwawa, n.k. kwa sababu kuharibu vitu hivyo ni sawa na kufanya uharibifu ardhini na Mwenyezi hapendi uharibifu.

Hivyo basi, wahanga wa migogoro ya kutumia silaha wamepata ulinzi mkubwa tangu mwanzoni mwa Uislamu, kwani Mtume (juu yake rehema na amani) yeye na makhalifa /viongozi/ wake waliokuja baada yake waliwapa umuhimu mkubwa sana wahanga wa vita, pasi na kuwabagua kwa misingi ya dini zao, utaifa au kabila zao.
Na endapo itatokea kwamba kuna ukiukwaji wa misingi iliyotajwa katika Qur'an na Hadithi, kuhusiana na kuwalinda wahanga wa vita, au kwenda kinyume na mwenendo wa maswahaba wa Mtume (juu yake rehema na amani) basi ubaya wa ukiukwaji huu usibebeshwe Uislamu, bali wabebeshwe wale waliokiuka haki za wahanga wa migogoro ya kutumia silaha, haki ambazo Uislamu wenyewe umewapa wahanga hawa kwa namna ambayo ni zaidi ya zilivyowekwa katika Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu.

**Sheikh Mkuu wa Al-Azhar**
**Muhammad Sayyid At-Twantwawiy**
**Tarehe 21/12/99**

# UTANGULIZI

Jumuiya ya Kimataifa imeshuhudia vita vikubwa hasa katika karne ya 20 ambapo silaha mpya za kiteknolojia ya kisasa zimetumika kwa ajili ya uharibifu. Na kama Sheria ya Kimataifa ya kisasa inakataza 'kufanya vitisho kwa kutumia nguvu dhidi ya usalama wa ardhi (nchi) au uhuru wa kisiasa wa nchi yoyote, au kutumia nguvu hiyo kwa malengo ambayo hayaendani na malengo ya Umoja wa Mataifa', na kwa kuwa sheria ya kuzuia matumizi ya nguvu ya jeshi (achilia mbali hali zisizo za kawaida ambazo imeruhusiwa kutumia nguvu ya jeshi) imekuwa ni sheria kali ambayo haifai kukiukwa au kufanya makubaliano yoyote yanayoenda kinyume na sheria hiyo.

Vivyo hivyo, Sheria ya Kiislamu hairuhusu kutumia nguvu ya jeshi isipokuwa katika hali ya kuzuia uadui, kupinga na kuondoa dhuluma, kutetea haki na wito wa Kiislamu pamoja na kuulinda dhidi ya uadui wowote ule. Ijulikane kwamba Uislamu haukuenea kwa upanga, ni kwamba, mapigano yaliyotokea huko nyuma yaliwalenga wale waliokuwa wakizuia wito wa Kiislamu usienee, bali wakaukataa na kuvunja ahadi.

Hivyo basi, Uislamu umekataza kata kata kumuua mtu ambaye amekataa kuingia katika Uislamu na kubaki katika dini yake, madamu mtu huyu atakuwa amekubaliana na waislamu kwamba atalinda amani ya Dola ya Kiislamu na kuheshimu makubaliano haya.

Na licha ya kwamba Uislamu (kwa rai ya wengi) pamoja na Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu vimekataza kupigana vita kwa lengo la kushambulia tu, lakini bado tunaona vita vinaendelea kuzuka na kuna waasi wanafanya ukiukwaji mkubwa wa misingi ya kisheria za kimataifa na Sheria ya Kiislamu pamoja na maadili ya kibinadamu. Ukiukwaji huu umepelekea kutafuta ulinzi wa lazima kwa wahanga wa vita, wakiwemo wafu, majeruhi, wagonjwa, mateka, waliozama, waliopotea, raia na vyanzo vya huduma za kijamii kwa maisha ya binadamu.

Kwa sababu yaliyowasibu wanadamu kupitia vita vingi hivi sasa viwe vya kimataifa au vya ndani miongoni mwa fedheha mbali mbali, khofu na matatizo vimewafanya wana fikra, wanazuoni, wanasiasa na taasisi mbali mbali za kimataifa na za ndani na nchi nyingi kutaka kumaliza au kukomesha athari za vita na upetukaji mipaka wa kijeshi na kuelekeza katika yanayoafikiana na vita

kwa upande mmoja na kwa upande mwingine misingi ya utu na ubinaadamu. Kwa misingi hiyo ni kuwa juhudi nyingi zilifanyika kuweka misingi na desturi na itifaki ya kulinda wahanga wa migogoro ya matumizi ya silaha, mali na vinavyomilikiwa ambavyo ni vya msingi vya kwao. Misingi hii imejengeka juu ya kunakili fikra mbali mbali na maadili mema na haswa ya utu wa mwanadamu katika Sheria za Umma za Kimataifa.

Misingi hii ya Sheria ya umma ya Kimataifa ambayo inalinda haki za mwanadamu wakati wa migogoro ya silaha istilahi ya 'Sheria za Kimataifa ya Kibinaadamu' na hivyo kwa kuongeza utu na ubinaadamu katika misingi ya Sheria ya migogoro ya matumizi ya silaha, matumizi ya istilahi hii inarudi kwa kamati ya kimataifa ya msalaba mwekundu. Istilahi hii imekuwa ndio istilahi inayokubalika zaidi sasa hivi, hakuna tofauti katika matumizi ya istilahi hii kwa kukusudia haki za mwanadamu wakati migogoro ya silaha.

Na yafuatayo ni maelezo mapana juu ya makusudio ya Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu, katika mtazamo wa sheria ya kisasa na Sheria ya Kiislamu.

## Maana ya Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ya kisasa

Msamiati (Sheria ya Kimataifa ya kibinadamu ),(kwa maana finyu) huwa unamaanisha mjumuisho wa sheria za kimataifa, zinazotokana na, ima mikataba au desturi zinazolenga kutatua matatizo ya binadamu yanayozuka moja kwa moja kutokana na migogoro ya ndani na ya kimataifa ya kutumia silaha, desturi na mikataba ambayo inazitaka kilazima na kwa sababu za kibinadamu pande mbili za mgogoro kutumia namna au mwenendo wa vita unaolinda vyanzo vya huduma za kijamii na watu ambao wamedhurika au wanaathirika kutokana na vita hivyo. Maana hii ndiyo iliyopitishwa na Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu.

Sheria ya Kimataifa ya kibinadamu ni mkusanyiko wa Mkataba wa The Hague na Mkataba wa Geneva. Mkataba wa The Hague umekusanya vifungu tofauti vya kisheria ambavyo vimepitishwa na Mikataba ya The Hague ya mwaka 1899 na 1907, ambayo imeweka haki na wajibu wa wapiganaji wakati wa kuendesha shughuli za kijeshi. Pamoja na mengineyo, Mkataba huo pia umekusudia kupunguza madhara ya vurugu na udanganyifu, kwamba zisivuke dharura za kijeshi. Hivyo basi, Mkataba wa The Hague, kwanza kabisa, umejikita katika kuweka misingi, kati ya nchi na nchi, kuhusiana na kutumia nguvu, wakati huo huo Mkataba wa Geneva umejikita katika kuwalinda, kuwaheshimu na

kuishi vizuri na wale wote ambao wamekuwa hawahusiki na vita na wale ambao hawashiriki katika matendo ya kiadui.

Mkataba wa Geneva ni mkusanyiko wa Mikataba minne ya mwaka 1949 inayohusiana na kuwalinda wahanga wa vita pamoja na Itifaki mbili za nyongeza ambazo zimepitishwa Geneva mwaka 1977

Msamiati (Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu) katika mtazamo wa Kiislamu

Misamiati ifuatayo: 'Sheria ya Umma ya Kimataifa' au 'Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu' haikutajwa katika Qur'an Tukufu wala katika vitabu vya Hadithi za mtume au vitabu vya urithi vya kiislamu kwa ujumla wake, kwa mfano vitabu vya Fiqhi, Siirah, vita, Tafsiri, Hadithi, Historia ya Kiislamu n.k.

Hili si jambo geni, kwa sababu misingi ya Sheria ya Kiislamu huwa ina sifa ya kueleza mambo kwa ujumla, kwa maana, misingi yake huwa inakusanya hukumu za dini na dunia. Ama inayokusanya hukumu za kidunia imekusanya mambo yanayosimamia mahusiano ya ndani, ambapo sheria hii huwa inajulikana kama Sheria ya Taifa ama sheria ya Nchi. Kama ambavyo Sheria ya Kiislamu huwa inasimamia mahusiano ya nje, kwa maana mahusiano ya Umma wa Kiislamu kwa mataifa mengine.
Ni imani ya waislamu kwamba, Sheria ya Kiislamu, ni sheria ya ulimwengu mzima ambayo inawataka binadamu kuitika wito wa tawheed (kuingia katika Uislamu), unawalingania katika hilo kwa hekima na mawaidha yaliyo mazuri. Zaidi ya hayo, Sheria ya Kiislamu pia inajenga uhusiano mzuri kati ya waislamu na wasiokuwa waislamu, iwe ni wakati wa vita au amani, kama ambavyo sheria hiyo, inaweka misingi ya lazima ambayo haifai kwenda kinyume nayo.

Kwa ujumla, katika hili, Sheria ya Kiislamu inatofautiana sana na sheria za kidunia, kwamba, kwenda kinyume na kanuni zake kunapelekea adhabu mbili papo hapo, adhabu ya kwanza ni hapa hapa duniani ambayo anaipitisha Kiongozi Muislamu kwa yule mwananchi wa kiislamu aliyekiuka Sheria hiyo, na adhabu ya pili, ni adhabu atakayoipata siku ya Kiama. Adhabu hizi mbili daima humfanya muislamu ashikamane na Sheria ya Kiislamu, sawa sawa sheria hizi ziwe zinahusiana na mahusiano ya muislamu kwa muislamu au muislamu kwa asiyekuwa muislamu.

Adhabu ya siku Kiama huwa inamfanya muislamu amtangulize Mwenyezi Mungu katika matendo yake, kwa kuamini kwamba, Mwenyezi Mungu anajua

mambo ya siri na ya wazi. Hivyo basi, mwenye kukiuka Sheria ya Kiislamu hata kama atafanikiwa kukimbia adhabu na majukumu ya dunia, hataweza kukimbia majukumu na adhabu ya siku ya Kiama.

Sheria ya Kiislamu na misingi yake, ambayo inazingatiwa kwamba inatoka kwa Mwenyezi Mungu, imejikita katika tabia njema na maadili ya kibinadamu. Kushikamana na tabia njema ni jambo la lazima katika Sheria ya Kiislamu. Na misingi ya tabia njema ni misingi haifai kukiukwa au kwenda nayo kinyume, kwa sababu mwenye kwenda nayo kinyume ataadhibiwa na Mwenyezi Mungu. Hii ndiyo tofauti iliyopo kati ya Sheria ya Kiislamu na Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ambayo inaangalia tu upande wa misingi ya tabia njema na kufanyiana wema ambayo haimlazimishi mtu kushikamana nazo, kwani anayeenda kinyume na misingi hiyo hana jukumu lolote la kimataifa (kwa maana haadhibiwi kwa kwenda kwake kinyume). Ongezea kwamba, Uislamu unawazingatia watu wote kuwa ni ndugu, hii inamaanisha kwamba, watu wote wapo sawasawa na asili yao ni Adam na Hawa (juu yao amani) Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu,

> ***"Enyi watu! Hakika Sisi tumekuumbeni kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumekujaalieni kuwa ni mataifa na makabila ili mjuane. Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliye mchamngu zaidi katika nyinyi....".*** *(49:13)*

Udugu wa kibinadamu uliowekwa na Uislamu, unawataka waislamu (wakati wa migogoro ya kutumia silaha) wasivuke mipaka ya dharura na kijeshi, na wakae vizuri na maadui zao, (wakishakuwa mateka) pasi na kuangalia dini zao, pia wawapatiwe ulinzi wa lazima, kwa sababu ubinadamu unaheshimu hadhi ya mwanadamu na unakataza jambo lolote ambalo linatweza uutu wake, kumdhalilisha, kumtisha, kuuminya uhuru wake au kuvunja mipaka ya imani yake.

Kwa msingi huo, Uislamu umewapa kinga, na kusisitiza juu ya kukaa vizuri na wahanga wa migogoro ya kutumia silaha (kama vile majeruhi, wagonjwa, maiti, waliozama baharini, mateka na raia), pia Uislamu umeweka kuwa ni lazima kulinda na kuheshimu na kuamiliana kwa utu pamoja na kulinda vyanzo vya huduma za kijamii na mali za raia. Kama ambavyo Uislamu umepangilia mienendo ya kupigana vita, kwamba vita inapozuka wapiganaji wasivuke dharura ya kijeshi, ni kwa sababu, katika Uislamu vita havikuhalalishwa hivi hivi tu, bali vimehalalishwa kwa kadri ya dharura tu.

Uchambuzi ufuatao utabainisha ni kiasi gani Sheria ya Kiislamu inawalinda wahanga wa vita katika maudhui katika kurasa zifuatazo. Kitu pekee tunachopenda kuelezea hapa ni kwamba, sheria za ulinzi kwa wahanga wa vita ambazo zipo katika Sheria ya Kimataifa, zimetungwa kati kati ya nusu ya karne ya kumi na tisa na ambazo zilithibitishwa rasmi mwaka 1949 baada ya kusainiwa Mikataba ya Geneva inayohusiana na kuwalinda wahanga wa vita. Lakini misingi ya Sheria ya Kiislamu inayohusu kuwalinda wahanga wa vita imekuwepo rasmi duniani tangu zaidi ya miaka 1400 iliyopita. Hivyo, Sheria ya Kiislamu imekuwa ni mfano wa kuigwa katika kuheshimu na kulinda haki za wahanga wa migogoro ya kutumia silaha ya ndani na ya kimataifa. Kwa muktadha huu, Sheria ya Kiislamu imeitangulia Sheria ya Kibinadamu ya Kimataifa, katika kuwalinda wahanga wa vita.

Kuna umuhimu wa kueleza kwamba marejeo ya Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu yanatofautiana na marejeo ya Sheria ya Kiislamu, marejeo ya Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu, kwa ujumla wake, ni kama marejeo ya Sheria ya Umma ya Kimataifa, yanatokana na mikataba na desturi za kimataifa, ambapo marejeo ya Sheria ya Kiislamu, inayowalinda wahanga wa vita inatokana na Qur’an Tukufu na Hadithi za Mtume Muhammad, marejeo haya mawili ndio misingi mikuu na marejeo mama ya sheria zote za Kiislamu.

Hivyo basi, kama hukumu ya jambo lolote lile haipatkani katika Qur’an, itatafutwa katika Hadithi Sahihi iliyopokewa kutoka kwa Mtume Muhammad (juu yake rehema na amani) ikipatikana itakuwa ndio marejeo ya hukumu ya jambo hilo, na kama marejeo ya hukumu fulani hayatapatikana katika Qur’an wala katika Hadithi, basi yatatafutwa kwa wasomi wabobezi wa Sheria ya Kiislamu wanaojua Qur’an na Hadithi, ambao wanatafuta asili ya Sheria na misingi yake ya ujumla ili kutoa hukumu hiyo. Wanachuoni hawa wa sheria huwa wanaitwa Mujtahidina (waliobobea) tena huwa wanajulikana kwa kufanya tafiti.

Kufuata utaratibu huu wa marejeo haya matatu (kwanza Qur’an kisha Hadithi na kisha wanazuoni wabobezi) umethibiti tangu enzi za Mtume Muhammad (juu yake rehema na amani) na utabakia hivi mpaka siku ya Kiama. Ushahidi wa hili ni ile Hadithi ya Mu’adh bin Jabal, (Mungu amridhie) kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (juu yake rehema na amani) alimtuma Mu’adh kwenda Yemen ili akawafundishe watu Qur’an na sheria za dini, kutatua na kutoa hukumu ya mizozo yao, Mu’adh (Mungu amridhie) aliulizwa na Mtume:

*“Utahukumu vipi pale kukizuka jambo? Akajibu, nitahukumu kwa kitabu*

*cha Mwenyezi Mungu, akaulizwa, kama hautapata -hukumu ya jambo hilo Kitabu cha Mwenyezi Mungu-? Akajibu, -nitahukumu- kwa Hadithi za Mtume, akaulizwa, kama hukupata? Akajibu, nitajitahidi kutafuta marejeo ya hukumu hiyo wala sitabweteka".*

Baada ya maelezo haya, tunaweza kuielezea Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu katika mtazamo wa Kiislamu kwamba ni: 'Vifungu vya Sheria vinavyotokana na Qur'an na Hadithi za Mtume au Ijtihad (rai) ya wanazuoni wabobezi wa Sheria ya Kiislamu, vifungu ambavyo vimelenga kutatua matatizo ya binadamu yanayozuka moja kwa moja kutokana na migogoro ya ndani au ya kimataifa ya kutumia silaha, na ambavyo vimeweka mipaka (kwa sababu za kibinadamu) mwenendo wa vita kwa namna ambayo inalinda vyanzo vya huduma za kijamii na watu walioathirika au kudhuriwa au wanaotarajiwa kudhuriwa na migogoro ya silaha'.

Kutokana na maelezo yaliyotangulia imeonekana wazi kwamba Sheria ya Kiislamu na Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ya kisasa zinafanana sana kwa kila kitu, tofauti pekee iliyopo kati ya sheria mbili hizi ni kuhusiana na marejeo yake, kwamba, majukumu ya Sheria ya Kimataifa ni ya kidunia tu, wakati majukumu ya Sheria ya Kiislamu ni ya kidunia na akhera.

Na kwa kuwa migogoro ya ndani ya kutumia silaha imepewa umuhimu mkubwa katika Jumuiya ya Kimataifa, na kwamba wahanga wake wamekuwa ni wenye kulindwa kwa mujibu wa Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu, na hasa hasa katika Itifaki ya pili ya mwaka 1977 iliyoambatanishwa katika Mikataba ya Geneva ya mwaka 1949, hivyo basi, tafiti yetu kuhusu wahanga wa migogoro ya kutumia silaha imegawanyika katika milango miwili:

**Mlango wa kwanza:** kuwalinda wahanga wa migogoro ya kimataifa ya kutumia silaha.

**Mlango wa pili:** kuwalinda wahanga wa migogoro ya ndani ya kutumia silaha

# MLANGO WA KWANZA

# ULINZI KWA WAHANGA WA MIGOGORO YA KIMATAIFA YA KUTUMIA SILAHA

## SURA YA KWANZA

# ULINZI KWA MAJERUHI, WAGONJWA NA WALIOKUMBWA NA MAAFA BAHARINI, KATIKA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU NA SHERIA YA KIISLAMU

# TAFITI YA KWANZA

# ULINZI KWA MAJERUHI, WAGONJWA NA WALIOKUMBWA NA MAAFA BAHARINI KATIKA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU

Neno (majeruhi na wagonjwa) katika Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu huwa linawakusudia wale wanajeshi au raia ambao wameacha kufanya matendo yoyote ya kiadui na kuhitajia msaada au huduma ya matibabu, kwa sababu ya kupatwa na mshituko, maradhi, au kuharibikiwa kimwili au kiakili. Maneno haya mawili (majeruhi na wagonjwa) yanajumuisha pia matukio ya kujifungua, watoto wachanga na watu wengineo ambao huenda wakahitaji msaada au huduma ya haraka, kama vile wenye mahitaji maalumu na wajawazito, ambao wameacha kufanya tendo lolote la uadui.

Ama neno (waliokumbwa na maafa na dhoruba baharini), hili huwa linawalenga wale wanajeshi au raia ambao hukumbwa na maafa baharini au katika maji yoyote na wameacha kufanya matendo ya kiadui, ni kwa sababu ya yale majanga yaliyowapata wao au meli na ndege zinazowasafirisha. Ijulikane kwamba, watu hawa watabaki kuwa ni wahanga wa baharini katika kipindi chote cha zoezi la kuwaokoa mpaka watakapopata mazingira mengine kwa mujibu wa Mikataba minne ya Geneva ya mwaka 1949, na Itifaki ya kwanza ya mwaka 1997, iliyoambatanishwa na Mikataba hii. Ni kwamba watabaki katika kinga hii kwa sharti kuwa hawaendelei kufanya matendo ya kiadui.

Kutokana na maelezo hayo yaliyotangulia, imebainika kwamba Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu imewapa ulinzi majeruhi, wagonjwa na waliokumbwa na majanga baharini, wawe ni wanajeshi au raia, kwa sharti kwamba wawe wameacha matendo ya kiadui. Na kwa kuwa hapo baadae tutaeleza, kwa kipekee, kuhusu ulinzi ambao Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu imetoa kwa

raia na vyanzo vya huduma za kijamii, hapa tutatosheka tu kwa kueleza kuhusu ulinzi uliowekwa kwa wanajeshi, majeruhi na wagonjwa, punde tu watapoweka silaha chini kama vile ambavyo wanavyotumia haki kulindwa iliyowekwa na Mkataba wa tatu wa Geneva kwa mateka wa vita, (pale tu wanapokua chini ya ulinzi wa mahasimu), mbali na ule ulinzi ambao wamepatiwa na mikataba miwili, wa kwanza na wa pili, Itifaki ya Kwanza ya mwaka 1977 inayohusiana na kuwapa ulinzi wahanga wa migogoro ya kimataifa ya kutumia silaha.

Na kama ilivyo kanuni ya jumla, kwamba yapasa kuwaheshimu na kuwalinda watu hawa na kukaa nao vizuri katika mazingira yote pasi na kuangalia ni wa upande upi, tena inatakikana wapatiwe huduma ya afya inayoendana na hali zao kwa haraka iwezekanavyo. Pia haifai kuwabagua kwa misingi yoyote ile isiyokuwa ya kimatibabu. Hivyo basi ni lazima kuwaangalia pasi na kuwabagua kwa utaifa wao, dini, au kabila lao. Na ni jukumu la upande unaotawala eneo la vita, kuwatafuta wahanga hawa na kuwalinda dhidi ya uadui na ubaya wowote, ambapo haifai kuwaua, kuwaadhibu na kuwatesa, kuwaweka rehani, au kuwapatia 'huduma zozote za kiafya ambazo haziendani na hali zao wala hazifanani na huduma za afya ambazo zinatolewa na upande mwingine kwa raia wake wanaoishi katika mazingira huru'. Inatahadharishwa vile vile na kwa hali ya kipekee kabisa kuwa, haifai kabisa watu hawa kukatwa viwiliwili vyao au kunyofolewa kwa lengo la kuvipandikiza katika mwili mwingine, au kuitumia miili yao kwa majaribio ya kimatibabu.

Pia haifai kuwaacha bila matibabu au kuwaacha wakumbwe na magonjwa ya milipuko au balaa. Na kwa kadri mazingira yatakavyoruhusu, ni lazima kwa pande mbili za vita kusimamisha mapigano, kusaini mkataba wa amani, au kufanya taratibu mbali mbali kwa lengo la kuhamisha na kubadilishana majeruhi waliopo kwenye viwanja vya vita na mfano wake. Kama ambavyo ni lazima kuandikisha maelezo yote ambayo yatasaidia kuhakiki taarifa ya kila mgonjwa, majeruhi, aliyezama au maiti wa upande wa hasimu.

Na ni lazima kuwalinda wahudumu wa taasisi za afya na dini wanaoambatana na wanajeshi, sawasawa watoa huduma hawa wawe ni wanajeshi au raia wa kawaida, iwe wanafanya kazi hiyo kwa mpito au kwa kudumu. Wanajumuishwa katika taasisi hizi, masheikh, mapadri na wengineo kutoka katika dini nyingine, wanaofanya kazi ya kutoa mawaidha na mahubiri na kuongoza ibada peke yake, wawe ni wanajeshi au raia. Inawezekana watu hawa kuwaambatanisha na majeshi au vitengo vya huduma za matibabu, iwe ni kwa mpito au kwa kudumu.

Katika jumla ya vitu vinavyoingia katika ulinzi huu ni pamoja na vyanzo vya huduma za kijamii za matibabu. ifahamike kuwa (Vyanzo vya huduma za kijamii za matibabu) vinavyokusudiwa kulindwa, ni viwanda na vitengo vyote vya tiba, viwe ni vya kijeshi au vya kiraia, kama vile hospitali, zahanati, kituo cha afya, kituo cha kuhifadhi na kuhamisha damu, vyuo vya udaktari, stoo za vifaatiba, maduka ya madawa yaliyowekwa kwa ajili ya vitengo hivi, sawa sawa yawe ni maduka yanayohama au ya kubaki sehemu moja tu. Vivyo hivyo yawe ni ya kudumu au ya muda maalum tu. Katika kinga hii vinaingia pia vitendea kazi vya matibabu vya kuhamishia wagonjwa na majeruhi na waliopatwa na majanga baharini, pia vitendea kazi vya kusafirisha watoa huduma wa taasisi za afya na dini, pamoja na vifaa vya matibabu ambavyo vinalindwa na Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu, sawasawa vitendea kazi hivi viwe ni vya baharini, nchi kavu au angani.

# TAFITI YA PILI

# ULINZI KWA MAJERUHI, WAGONJWA NA WALIOKUMBWA NA MAJANGA BAHARINI, KATIKA SHERIA YA KIISLAMU

Sheria ya kimataifa ya kulinda majeruhi, wagonjwa, mateka na wengineo miongoni mwa wahanga wa migogoro ya kutumia silaha, imewekwa hivi karibuni ikilinganishwa na muda au umri wa ulinzi katika Sheria ya Kiislamu (ambayo ipo muda mrefu zaidi). Kwa sababu Uislamu tangu ulipoanza uliweka ulinzi kamili kwa majeruhi, wagonjwa, waliozama na wengineo miongoni mwa wahanga wa vita.

Hivyo basi, majeruhi, wagonjwa na waliozama wana haki ya kupewa ulinzi pindi tu watakapotangaza kuingia katika Uislamu, ni kwa sababu Uislamu unakataza kuua adui ambaye ametangaza kusilimu kwake, (sawa sawa asilimu wakati wa vita au wakati wa amani), mtu huyo hafai kuuawa. Na ushahidi wa jambo hili, ni Hadithi iliyopokewa na Al-Bukhariy kwamba: Mikidadi bin 'Amr Al Kindiy -na huyu Mikidadi ni miongoni mwa watu walioshiriki katika vita vya Badri wakiwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu (juu yake rehema na amani) alisema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, unaonaje (wakati wa vita kati ya waislamu na wasiokuwa waislamu) kama nitakutana na mtu katika wale wasiokuwa waislamu, tukapigana, naye akaukata mkono wangu kwa upanga, kisha akajikinga na mti kwa kunikimbia mimi, na akasema: Nimeingia katika Uislamu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, hivi nimuue baada ya kusema hivi? Naye Mtume wa Mwenyezi Mungu (juu yake rehema na amani) akajibu 'Usimuue'.

Na kama maadui hawakusilimu, na wakakubali kuwapa waislamu kiasi cha pesa, kama malipo ya kulindwa kwao, na kuwatetea pamoja na kuhifadhi mali zao na kuishi kwa uhuru, basi Uislamu unawapatia watu hawa ulinzi huo na unakataza kata kata kuwaua.

Ushahidi juu hili ni Hadithi iliyopokewa na Ahmad, Muslim, Bin Maajah na At-Tirmidhiy, kutoka kwa Sulayman bin Buraydah, naye kapokea kutoka kwa baba yake, amesema: 'Alikuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu pindi anapomteua mtu kuwa Mkuu wa Majeshi au Kikosi, akimuusia kheri, katika yale ambayo huwa anaiusia nafsi yake na anayowausia waislamu walio pamoja naye, kisha huwa anasema:

"*Piganeni kwa jina la Mwenyezi Mungu, katika njia ya Mwenyezi Mungu, mpigeni mwenye kupinga, piganeni vita, wala msiibe mali, msivunje ahadi, msikatekate maiti, wala msiue mtoto mdogo, na ukikutana na maadui zako wape hiari ya mambo matatu, wakichagua jambo lolote kati ya hayo wakubalie na usipigane nao, -kwanza- walinganie – wafahamishe (kuhusu Uislamu) na uwatake waingie katika ya Uislamu kwa hiari yao-, wakikubali (kuingia katika Uislamu) basi wakubalie na usipigane nao, wakikataa -hilo jambo la kwanza- basi waambie watoe kodi (jizya) wakikubali basi wakubalie na usiwapige vita, wakikataa -hilo jambo la pili- basi (la tatu na la mwisho) Omba msaada kwa Mwenyezi Mungu na upigane nao*".

Katika maelezo haya tunaweza kufahamu kwamba, Uislamu unakataza kumuua adui pindi tu atakapotangaza kusilimu, na endapo hakusilimu lakini pakapita suluhu kati ya pande mbili, kwamba kuna malipo watapatiwa waislamu kwa ajili ya kuwalinda wasiokuwa waislamu, kuwatetea na kulinda haki na uhuru wao, suluhu hii huwa ndio kinga ya kulinda damu ya adui, na kama ikiwa hakuna budi na vita, kwa sababu adui ana tabia ya kuwavizia waislamu na kuwafanyia uadui, muda huu vita itakuwa kitu cha dharura, na dharura huwa inakadiriwa ukubwa wake, na hapo ndipo Uislamu unapokataza kuua wanawake, watoto na wengineo katika wale wasiopigana, namna hiyo hiyo Uislamu unakataza kuvunja ahadi na adui au kukatakata maiti au kuwaadhibu wagonjwa na majeruhi.

Ushahidi wa kukataza kuwatesa wagonjwa, majeruhi, waliozama baharini au wengineo miongoni mwa wahanga wa vita, ni kauli yake Mtume (juu yake rehema na amani) aliposema: "*Hakika, Mwenyezi Mungu atawaadhibu siku ya Kiama wale ambao wanawatesa watu duniani*". Haya ni maelezo ya jumla, yanakataza kuwatesa watu katika vipindi vyote viwili, kipindi cha vita na kipindi cha amani, na pia hawa watu wawe ni waislamu au sio waislamu. Kwa muktadha huu, Uislamu unakataza kuwatesa majeruhi, wagonjwa, waliokumbwa na majanga baharini na maadui ambao hawawezi hata kujitetea wao wenyewe.

Na miongoni mwa dalili za kuonesha kwamba ni lazima kuwapa ulinzi majeruhi, wagonjwa na waliozama, ni kwamba kuwaua watu hawa, kuwatesa au hata kuvunja heshima ya uutu wao hakusaidii kuleta manufaa yoyote ya kijeshi, kwa sababu hawa wamekuwa hawawezi tena kupigana vita, na kwamba kuwaua au kuwaadhibu na kuwatesa kunazingatiwa kuwa ni kuvuka hali ya dharura, na huko ndiko kufanya uharibifu ardhini kulikokatazwa kwa mujibu wa sheria,

***"...wala msiasi katika nchi mkafanya uharibifu."*** *(2:60)*

Na ikiwa Uislamu unakataza kuua wanawake, watoto, wazee na viongozi wa dini kwa sababu ya kutoshiriki kwao katika vita, na kwa kuwa hawasababishi udhia au madhara yoyote, basi hata majeruhi, wagonjwa na waliozama nao wameshashindwa kupigana na wamekuwa sio sehemu tena ya nguvu ya jeshi lao, na kwa muktadha huu wanakuwa sawa sawa na wale wasiopigana kama vile wanawake, watoto, mapadri na masheikh pamoja na wazee, hivyo basi haifai kuwaua kwa mujibu wa Sheria ya Kiislamu.

Ushahidi mwingine kwamba haifai kuwaua majeruhi na wagonjwa, pindi tu watakapoacha kufanya matendo ya kiadui, ni ule msimamo aliochukua Mtume (juu yake rehema na amani) kwa watu wa Makka, siku ile alipoifungua, kwani hakumgusa mtu yeyote wala mali yoyote kwa ubaya, bali alitangaza mtangazaji wake: Chonde chonde asiuliwe Majeruhi, wala asifuatwe mwenye kukimbia, na wala asiuliwe mateka, na mwenye kufunga mlango wake basi huyo amesalimika. Sheria hii inatumika katika vita vyote.

# TAFITI YA TATU

# UWIANO ULIOPO KATI YA SHERIA YA KIISLAMU NA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU

Sheria ya kimataifa ya kibinadamu haina tofauti na yaliyomo katika Sheria ya Kiislamu kuhusiana na kukaa vizuri na majeruhi, wagonjwa na waliokumbwa na majanga majini. Kwa sababu Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu imeweka kwamba, ili wahanga hawa walindwe basi ni sharti wawe wameacha kufanya matendo ya kiadui, na ndiyo sharti hiyo hiyo ambayo Sheria ya Kiislamu imeiweka kwa ajili ya kuwalinda watu hawa. Na kama Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu imekataza hivi karibuni kuwaua au kuwaadhibu na kuwatesa wahanga hawa, basi Sheria ya Kiislamu nayo imeweka katazo hilo tangu zaidi ya miaka 1400 iliyopita.

Pia Sheria ya Kiislamu haitofautiani na Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu kuhusiana na kuwapatia watu hawa huduma za afya, kwa sababu Mtume (juu yake rehema na amani) aliwasisitiza sana maswahaba wake juu ya kuwakirimu mateka wao. Na ijulikane kwamba kuwafanyia ukarimu mateka ni pamoja na kuwapatia majeruhi na wagonjwa huduma za afya, na si kuwapa chakula, mavazi na malazi tu peke yake.

Na kwa kuwa ni lazima kuwapatia watu hawa huduma ya afya, basi ni wajibu wa kisheria pia kulinda vitengo na vyanzo vya afya ili lengo la kutoa huduma za afya likamilike, (*kwa sababu ni lazima kufanya jambo ambalo linapelekea kutimiza wajibu*). Vivyo hivyo, ni lazima kuwalinda viongozi wa dini wanaoambatana na majeshi, kwa muda wote ambao hawashiriki katika mapigano, na hili ni katazo la wazi kabisa kutoka kwa Mtume (juu yake rehema na amani) na viongozi waliokuja baada yake, kwamba haifai kuwaua viongozi wa dini ambao hawashiriki mapigano vitani.

Hivyo basi, hakuna tofauti kati ya Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu na Sheria ya Kiislamu katika maudhui hii.

# SURA YA PILI

# ULINZI KWA MATEKA KATIKA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU NA SHERIA YA KIISLAMU

Sura hii ina tafiti tatu:

**Tafiti ya kwanza:** Je ni nani hao mateka wa vita, katika Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu na Sheria ya Kiislamu.

**Tafiti ya pili:** Ulinzi kwa mateka, katika Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu.

**Tafiti ya tatu:** Ulinzi kwa mateka, katika Sheria ya Kiislamu.

# TAFITI YA KWANZA

# MAKUSUDIO YA MATEKA WA KIVITA KATIKA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU, NA SHERIA YA KIISLAMU

## 1. Makusudio ya 'Mateka wa vita' katika Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu

Kuna makundi mawili ya watu ambao wana sifa ya kuitwa mateka wa vita

**Kundi la kwanza:** wapiganaji rasmi na wanaofanana nao.
Mpiganaji rasmi ana hadhi maalumu ya kisheria iliyowekwa kwa mateka. Anastahiki hadhi hii pindi tu atakapoacha kupigana, ima ameacha kupigana kwa kupenda kwake au pasi na kupenda kwake, kwa mfano atakapoamua kuweka silaha chini na kusalimu amri, hapo atakuwa ameacha kupigana kwa kupenda kwake, lakini kama atakuwa ameacha kupigana kwa sababu amekuwa ni majeruhi asiyejiweza, hapo atakuwa ameacha kupigana pasi na kupenda kwake.

Katika hali zote mbili atastahili hadhi maalumu ya mateka. Ijulikane kuwa, mpiganaji rasmi anayekusudiwa hapa ni yule (ambaye ana vigezo vilivyowekwa na Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu, miongoni mwa vigezo hivyo ni pamoja na kwamba mpiganaji huyu atakuwa na wajibu wa kuheshimu sheria na desturi za vita).

Kama ambavyo wasifu huo umeongeza kuwa inawahusu pia wapiganaji rasmi wanaofuata serikali au utawala ambao hautambuliki na nchi iliyowazuia.

Itifaki ya Tatu ya Geneva ya mwaka 1949 imeongezea kwamba, wafuatao wanazingatiwa kuwa ni mateka wa vita:

**a.** Wanaharakati wapiganaji wa vikundi vya kimfumo vya upinzani ambao wanafanya kazi ndani ya nchi yao, hata kama nchi yao itakuwa imevamiwa, kwa sharti kwamba wanaharakati hawa wawe na vigezo na masharti kama yalivyokuja kwenye Ilani ya The Hague ya mwaka 1907, nayo ni :

- Wapiganaji hawa wawe chini ya kiongozi, anayewajibika kwa raia wake.
- Wawe na alama maalumu inayoweza kuwatambulisha hata kama watakuwa mbali.
- Wabebe silaha zao wazi wazi.
- Waheshimu sheria na desturi vita.

**b.** Wananchi wa eneo ambalo bado halijatekwa, ambao walikuwa wakielekea kupambana na majeshi yaliyovamia nchi yao, kwa sharti kwamba wananchi hawa wawe wamebeba silaha wazi wazi pamoja na kuheshimu sheria na desturi za vita.

Itifaki ya kwanza ya Geneva ya mwaka 1977 iliyoambatanishwa na Mikataba ya Geneva ya mwaka 1949 nayo imeeleza kwamba, sheria hii (inahusika pia katika hali ambazo zimeelezwa katika kifungu cha pili cha pamoja na Mikataba hii). Na hali zilizotajwa hapo juu zinajumuisha pia migogoro ya kutumia silaha, ambayo kwa kawaida huwa mataifa yanapambana dhidi ya utawala wa kikoloni, uvamizi wa kigeni au dhidi ya serikali zenye mfumo wa ubaguzi. Mataifa haya huwa yanapambana huku wakitumia (Haki ya watu katika kufanya maamuzi yao) haki ambayo inatambuliwa na Mkataba wa Umoja wa Mataifa, kama vile inavyotambulika katika tangazo la misingi ya sheria ya kimataifa inayohusiana na mahusiano mema na ushirikiano kati ya nchi na nchi kwa mujibu wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa.

**Makundi mengineyo ambayo yana sifa ya kuitwa mateka wa vita**

Yapo makundi kadhaa ambayo yana sifa ya kuitwa mateka wa vita, ambayo hayazingatiwi kuwa ni wapiganaji, nayo ni:

**a.** Raia wanaoongozana na majeshi, ni pamoja na waandaaji chakula, wafanyakazi, na makundi ya Sanaa ambayo huwa yanafanya kazi ya kuwaburudisha wanajeshi, na makundi yanayoongozana na usafirishaji wa ndege za kivita, na waandishi wa habari za vita. Itambulike kuwa, watu hawa wanajumuishwa na mateka kwa sharti moja tu, kwamba wawe wamepatiwa vibali na vitambulisho kutoka kwa wanajeshi wanaoongozana nao, kwa namna na mfano ambao umewekwa katika Mkataba wa Tatu wa Geneva wa mwaka 1949.

**b.** Wafanyakazi wa meli, wakiwemo viongozi, mabaharia na wasaidizi wao

katika usafirishaji wa ndege za kiraia ambao wako chini ya moja ya pande za vita, na ambao hawapati muamala mzuri kwa mujibu wa sheria nyingine za kimataifa.

## 2. Makusudio ya Mateka wa vita katika Sheria ya Kiislamu

Katika Sheria ya Kiislamu, neno Mateka wa vita huwa linawakusudia wale wapiganaji wasiokuwa waislamu wakitekwa na waislamu hali ya kuwa ni wazima. Ni wale watu ambao wanaweza kupigana na wameshiriki moja kwa moja katika matendo ya kiadui dhidi ya Dola ya Kiislamu. Hivyo basi, raia wa kawaida, wawe ni watu wazima au vijana ambao hawapigani, hawaingii katika orodha hii ya mateka, vivyo hivyo wanawake, watoto, viongozi wa dini na wengineo ambao hawashiriki katika vita. Kwa muktadha huu, ni lazima kwa kila mtu ambaye hashiriki katika matendo ya kiadui, wala haingii katika orodha ya mateka, apewe haki za raia wa kawaida.

# UWIANO ULIOPO KATI YA SHERIA YA KIISLAMU NA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU

Hakuna tofauti baina ya Sheria ya Kiislamu na Sheria ya Kimataifa Kibinadamu kuhusiana na kwamba, wanaoshiriki katika matendo ya kivita wanazingatiwa kuwa ni mateka ambao watahitaji wapate ulinzi (pale watakapokamatwa). Hivyo inapasa kuwalinda katika vita inayotokea kati ya nchi na nchi, au kati ya nchi na kundi fulani ambalo si nchi muda wa kuwa vita vyao vinapelekea katika kufanya maamuzi ya mwelekeo fulani wa maisha yao.

# TAFITI YA PILI

# ULINZI KWA MATEKA KATIKA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU

## UTANGULIZI

Mateka yeyote wa vita hawi chini ya utawala wa jeshi ambalo limemteka nyara, bali huwa yuko chini ya utawala wa nchi ya wanajeshi waliomteka. Na ni lazima kwa nchi hiyo kuwaheshimu mateka ambao wako chini ya uongozi wao, kuwapa ulinzi pamoja na kukaa nao vizuri. Kwani mtu kutekwa nyara haimaanishi kwamba anatakiwa kupewa adhabu au kulipiziwa kisasi, bali hiyo ni njia tu ya kumzuia mateka huyo asiweze kufanya maudhi au madhara yoyote. Hivyo basi, kumchukulia mateka hatua kali zozote ambazo zinavuka lengo hili kunazingatiwa kuwa si jambo la lazima.

Mkataba wa Geneva wa mwaka 1949 unaohusiana na kukaa vizuri na mateka umeelezea pia madhumuni haya, na umewapa kinga mateka tangu wanapoangukia kwenye hali hii ya kutekwa mpaka watakapoachiwa huru na kurejea katika majumba na miji yao. Namna hiyo hiyo, Sheria ya Kiislamu imewapa ulinzi mateka kwa namna ambayo ni zaidi ya ulinzi waliopatiwa na Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu, na yafuatayo ni maelezo mapana zaidi kuhusiana na hilo:

## KINGA WAKATI WA MTU KUWA NI MATEKA

Imekatazwa kata kata kuua mateka (pindi tu anapoweka silaha chini na kujisalamisha kwa adui) na inabidi nchi iliyomzuia mateka yeyote impatie vitambulisho na vielelezo vya kuthibitisha uraia wake, wala haifai kumvua nyota zake, nishani na uraia wake, pia haifai kumpokonya vitu vyovyote vya kumbukumbu au vitu ambavyo mateka anavithamini.

Na ni wajibu wa nchi ambayo imeteka nyara kumsafirisha mateka haraka iwezekanavyo, impeleke katika kambi ambazo ziko mbali kabisa na sehemu za vita, ili kumkinga dhidi ya hatari ya shughuli za kijeshi. Na ni vema kuzingatia kwamba wakati wa kuhamishwa kwao wahamishwe kwa njia ya kibinadamu na itakayowakinga dhidi ya hatari.

### Kufanya mahojiano na mateka

Ni wajibu wa mateka mwenye cheo chochote cha kijeshi, kujibu maswali maalumu, nayo ni yale yanayohusiana na jina lake kamili, tarehe yake ya kuzaliwa, cheo chake cha jeshi au kikosi chake, au nambari yake ya serial. Na endapo mateka atagoma kujibu maswali haya, basi itakuwa ni sahihi kumnyima baadhi ya hadhi, stahili na vipaumbele fulani vinavyotolewa kulingana na cheo au nafasi yake ya kijeshi.

Haifai kwa nchi iliyomteka kuanza kumuadhibu na kumtesa au kumlazimisha kufanya kitu chochote ili aweze kutoa maelezo fulani.

## KINGA ILIYOWEKWA KWA MATEKA WAKATI WA ZOEZI LA UTEKAJI

### 1. Haki ya kufanyiwa muamala wa kibinadamu

Kifungu cha (13) cha Mkataba wa Tatu wa Geneva, kimeeleza kuhusu ulazima wa kuwafanyia mateka muamala wa kibinadamu katika nyakati na mazingira yote, kama vile ambavyo kimekataza kufanya jambo lolote litakalosababisha kifo cha mateka ama kuifanya afya yake kudorora ama kuwa hatarini. Hivyo basi, haifai kukata kiungo chake chochote au kukifanyia majaribio ya kimatibabu au kisayansi kwa namna ambayo inapingana na taratibu za kitengo cha matibabu kinachowahudumia mateka.

Na kwa namna yoyote ile, imekatazwa kumlipiza mateka kisasi, kwani kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria, na kunapingana na misingi ya Sheria ya Kimataifa ya kutetea haki za mateka wa vita ambazo ni maalum na zile haki za nchi wanayotoka mateka.

### 2. Haki ya kuheshimu utu na hadhi

Mateka wote wa vita, na katika mazingira na nyakati zote, wana haki ya kuheshimiwa utu na hadhi zao, na wana haki ya kubaki na uraia wao waliokuwa nao kabla ya kutekwa, ambapo wataendelea kutumia haki zao za

uraia kwa mujibu wa sheria za nchi zao. Kwa upande mwingine, haifai kwa nchi iliyowateka, kuweka vikwazo vya aina yoyote dhidi ya kutumia haki hizi, isipokuwa kwa kiasi ambacho huenda kikatumika kwa sababu za kimateka.

Na ni lazima mateka wa kike wafanyiwe muamala mwema sawa na ule ambao hufanyiwa wanaume, muamala ambao unaendana na jinsia yao kwa namna ambayo haitii dosari heshima yao. Pamoja na hayo, ni lazima kuwatengea wanawake sehemu zao maalumu.

## 3. Haki ya kupata huduma ya afya na matibabu

Kifungu cha 15 cha Mkataba wa Tatu wa Geneva kinaeleza kuwa, ni wajibu wa nchi iliyomteka nyara kumpatia mateka huduma ya afya na matibabu ambayo inahitajika kwa hali yao ya kiafya.

Kifungu cha 29 cha mkataba huo huo kinaitaka nchi iliyoteka nyara kuchukua hatua za lazima za kiafya, kwa kuzingatia usafi na afya katika kambi, pamoja na kuzuia kuenea kwa maradhi na magonjwa ya mlipuko, na kwamba, mateka watengewe sehemu safi za afya, na wanawake nao, watengewe sehemu zao kando.

Na imeelezwa pia kwamba katika kambi zote, ni lazima kuwe na zahanati zenye chakula na dawa muwafaka na mnasaba kwa magonjwa mbali mbali sambamba na kuwasafirisha mateka kwenda katika hospitali za raia au za jeshi, endapo hali zao za kiafya zitahitaji hivyo. Gharama zote za matibabu zitasimamiwa na nchi ambayo imewashikilia mateka hao, zikiwemo gharama za vifaa vya matibabu yao. Na ni lazima kufuatilia na kuchunguza maendeleo ya afya zao kwa kila mwezi, ili kuhakikisha kuwa hawana maradhi ya kuambukizana.

## 4. Haki Ya Usawa Katika Muamala

Kwa mujibu wa kifungu cha 16 cha Mkataba wa Tatu wa Geneva, ni lazima kwa nchi iliyowazuia mateka wa vita kuwafanyia usawa baina yao bila ubaguzi wowote, iwe kwa msingi wa kijinsia, itikadi ya dini, siasa au kwa misingi yoyote inayofanana na hiyo. Na nchi iliyowaweka mateka kizuizini italazimika kufanya usawa huu pale hadhi na hali za mateka zitakapokuwa zinafanana, kwamba usawa huu hautaharibu mazingatio ya vyeo vya kijeshi, au hautaingilia haki za baadhi ya mateka ambao hali zao za kiafya, miaka au sifa na vigezo vyao vya kitaaluma haviruhusu kuchanganyika na mateka wengine.

## 5. Haki ya uhuru wa kuabudu

Mkataba wa Tatu wa Geneva unaitaka nchi iliyowazuia mateka kuwapa mateka hao, uhuru wa kuabudu, kulingana na mfumo uliowekwa na mamlaka ya jeshi ambayo ina jukumu la kutenga sehemu za kufanyia ibada. Pia ni lazima haki hii wapatiwe viongozi wa dini ambao walikuwa kizuizini kwa ajili ya kuwasadia mateka, ili waweze kufanya ibada na mateka ambao wapo katika Imani moja, kama ambavyo inapasa kuwasambaza viongozi hawa wa dini katika kambi na vitengo tofauti vya kambi ambazo zina mateka wanaofanana nao kiimani na lugha.

## 6. Haki ya kujishughulisha kiakili na mwili

Kifungu 38 cha Mkataba wa Tatu wa Geneva kinaeleza kwamba ni lazima kwa nchi ambayo imewaweka mateka kizuizini kuwahamasisha mateka hao kujishughulisha kiakili na kimwili, kushiriki katika mambo ya kitamaduni, mazoezi, michezo na mashindano. Na katika hili ni haki ya kila mateka kuchagua kitu anachokipenda, kama ambavyo ni jukumu la lazima kwa nchi iliyowaweka kizuizini kuwatengea eneo na vifaa husika, sawasawa iwe ndani au nje ya kambi .

## 7. Haki ya kujikimu na kupata mahitaji ya msingi

Miongoni mwa haki za mateka ni pamoja na kupata sehemu ya kulala, kula na mavazi.

### (a) Haki ya malazi

Ni lazima sehemu za kuwaweka mateka zifanane sawa sawa na kambi za jeshi ambalo nchi yake imewaweka watu kizuizini, na kwa kipekee ni lazima sehemu za kuwalaza mateka ziwe na vigezo vya afya, pia patengwe sehemu za kukaa maafisa wa jeshi kulingana na vyeo vyao vya kijeshi, sambamba na kuandaa sehemu maalumu za wanawake katika kambi ambazo kuna mchanganyiko wa mateka wanaume na wanawake.

### (b) Haki ya chakula

Ni lazima mateka wapate chakula cha kutosha chenye kiwango na ubora kama ambavyo ni lazima kwa mateka wanofanya kazi za ziada wapewe chakula cha nyongeza. Pia ni lazima wapatiwe maji pamoja na kuandaliwe sehemu maalumu ya kula. Na haifai kabisa kupunguza chakula chao walau kidogo, eti kwa ajili ya kuwatesa tu.

Na kwa kadri iwezekanavyo, inapasa mateka waruhusiwe kuandaa chakula chao jikoni, pia waruhusiwe kula vyakula hivyo. Na kujengwe migahawa katika kambi zote za mateka ili waweze kupata mahitaji yao ya vyakula na vinywaji na mahitaji yao ya kila siku. Kadhalika haifai kupandisha bei za vyakula zaidi ya ile bei ya soko la kawaida.

**(c) Haki ya mavazi**

Ni lazima mateka wawe na nguo za kutosha zikiwemo nguo za nje na za ndani, pamoja na soksi. Tena wawe na mavazi ambayo yanaendana na mazingira ya eneo wanalokaa. Pia mateka waruhusiwe kuvaa sare zao za jeshi pamoja na kubandika nyota na nishani zao. Na endapo nchi iliyowaweka mateka kizuizini itaokota rundo la nguo za maadui ambao ndio mateka wenyewe, nchi hiyo itatakiwa kuwapatia nguo hizo, endapo nguo za mateka hao zitakuwa zimechakaa. Na ni lazima kwa nchi iliyowaweka mateka kizuizini iwe makini kufuatilia matengenezo ya nguo zao na kuwapa zingine, na iwapatie nguo maalumu makundi ya wale ambao hufanya kazi, kila kundi lipate nguo zinazoendana na kazi zao.

## 8. Haki ya mateka kufanya mawasiliano nje ya kambi

Punde tu mtu anapogeuka kuwa ni mateka, na ndani ya kipindi kisichozidi wiki moja tangu kuingia kambini, hata kama itakuwa ni kambi ya mpito tu, vivyo hivyo kama mateka ataugua au kuhamishiwa kambi nyingine, ni haki ya mateka huyo kuruhusiwa kuwasiliana moja kwa moja (kwa maandishi) na familia yake na pia kuwasiliana na Kituo Kikuu cha Mateka wa Vita au Wakala wa Kutafuta Mateka na Waliopotea ambao hufanya kazi chini ya Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu (Geneva).

Utaratibu utakaofanyika ni kuwa Mateka atajaza taarifa zake katika fomu (ikiwezekana) inayofanana na ile iliyoambatanishwa na Mkataba wa Tatu wa Geneva wa mwaka 1949, ambapo ataweza kuifahamisha familia na ndugu zake kuhusu kutekwa kwake na hali yake ya kiafya. Kwa upande mwingine, nchi iliyomuweka mateka kizuizini itatakiwa imruhusu kupokea barua na kadi pamoja na vifurushi vya chakula, madawa na vipeperushi vya dini au elimu.

# TAFITI YA TATU

# ULINZI KWA MATEKA KATIKA SHERIA YA KIISLAMU

## UTANGULIZI

Misingi ya kuzingatia utu na ubinadamu iliyopo katika Uislamu, inaakisi muamala mzuri ambao Uislamu umeuweka kwa mateka, kama vile kuwataka waislamu kuwa na huruma, kusamehe, hisani, na kuheshimu utu wa mwanadamu, na kumfanyia uadilifu, na udugu wa kibinadamu mateka.

Uislamu umewajibisha kwamba ni lazima mateka wapewe muamala wa kibinadamu na kuheshimu haki na uhuru wao, tangu wanapotekwa nyara na waislamu mpaka kurudi nyumbani kwao kwa ndugu zao.

Pia katika Uislamu, mateka hawawi chini ya jeshi au kikosi ambacho kimewateka, bali wanakuwa chini ya Rais wa Dola ya Kiislamu au mwakilishi wake. Na sheria hii inafanana kabisa na Kifungu cha 12 cha Mkataba wa Tatu wa Geneva.

Ufuatao ni ufafanuzi wa muamala mzuri ambao Uislamu umewataka waislamu kuwafanyia mateka wa vita.

## KUWAPA MALAZI MATEKA WA KIVITA

Wakati wa Mtume (juu yake rehema na amani) Waislamu walikuwa hawatengi kambi ama majengo maalumu ya kuhifadhi mateka kama ambavyo tunashuhudia katika vita vya kisasa, ni kwa sababu kipindi hicho kilikuwa ndio kwanza kunaanzishwa Dola ya Kiislamu. Ila ni ukweli usiopingika kwamba mateka walineemeka sana chini ya utawala ule wa Kiislamu, kwani walipata makazi mazuri ndani ya kipindi chote walichokuwa ni mateka chini ya Dola ya Kiislamu.

Kipindi hicho hali ilikuwa hivi, ima Mtume mwenyewe alikuwa anawagawanya mateka kwa waislamu, ili wakae nao katika nyumba zao, ama mateka hao walikuwa wakiwekwa msikitini mpaka ile hali yao ya kuwa mateka itakapoisha.

Ni vema ieleweke kwamba Uislamu haukatazi kutenga kambi au majengo maalumu ya mateka ambayo yatakuwa na vigezo vya usalama na afya vilivyotajwa katika Mkataba wa Geneva, ni kwa sababu Mtume (juu yake rehema na amani) aliwaamrisha maswahaba wake kuwakirimu na kukaa vizuri na mateka wa Vita vya Badr.

Ongezea kwamba, kukaa vizuri na mateka hakuishii kwenye kula na kunywa tu peke yake, bali ni pamoja na kuwapa malazi mazuri na kila ambacho kinahesabika kuwa ni muamala mzuri, ambao unaendana na mwanadamu aliyetukuzwa na Mwenyezi Mungu katika kitabu chake kitukufu aliposema ***"Na hakika tumewatukuza wanaadamu..." (17:70)*** yaani mtu yeyote, pasi na kuangalia rangi yake, utaifa au jinsia yake.

## KUWAPA CHAKULA MATEKA

Ikiwa Mkataba wa Geneva umewajibisha kuwapa mateka chakula bora na cha kutosha, kinachofanana na kile wanachokula wanajeshi wa nchi iliyofanya utekaji, basi Uislamu umewapa mateka mazuri zaidi ya hayo. Na hii inaonekana wazi katika yale waliyokuwa waislamu wakiwafanyia mateka wa Vita vya Badri, kwani waislamu walikuwa wakiwatanguliza mateka kwenye chakula japokuwa walikihitaji na kukipenda sana chakula hicho.

Jambo hili lilitokea ikiwa ni utekelezaji wa amri ya Mtume (juu yake rehema na amani) iliyowataka waislamu kuwakirimu mateka. Kutokana na uzuri wa utekelezaji wa mafundisho haya, Mwenyezi Mungu alishusha neno lake akiwasifu na kusema,

> ***"Na huwalisha chakula, juu ya kukipenda kwake, masikini, na yatima, na wafungwa" (76:8)***

Pia palishuhudiwa, Mtume (juu yake rehema na amani) akiletewa mateka, kisha na yeye akamkabidhi mateka huyo kwa muislamu na kumwambia "*Mtendee wema huyo*". Aidha Mtume alishawahi kusema "*Mateka wako ni sawa na mtu anayekudai, hivyo mtendee wema mateka wako*".

Kuwafanyia wema mateka ni pamoja na kuwalisha, ni miongoni mwa mambo yaliyotajwa katika Hadithi ya Mtume (juu yake rehema na amani) aliposema "*Mwachieni huru mateka, na mlisheni mwenye njaa, na tembeleeni wagonjwa*". Hadithi hii imepokewa na Al-Bukhari kutoka kwa Abu Mussa (Mungu amridhie)

Hivyo imebainika wazi kwamba katika mambo yaliyosisitizwa sana na Uislamu ni pamoja na kumlisha mwenye njaa yeyote yule, mateka na wasiokuwa mateka.

Ikumbukwe, pindi mtu aitwae Thamama bin Athal alipokuwa ni mateka chini ya waislamu, waislamu hao hao ndio waliokuwa wakimletea chakula na maziwa kutoka nyumbani kwa Mtume (juu yake rehema na amani).

Imam Ahmad na Muslim wamepokea Hadithi iliyosimuliwa na Imran bin Haswiin amesema kuwa kabila la Thaqiif liliingia mkataba wa ushirikiano na kabila ya Bani 'Aqeel, basi kabila ya Thaqiif wakawateka watu wawili wa Mtume (juu yake rehema na amani). Kwa upande mwingine, Mtume naye (juu yake rehema na amani) akamteka mtu mmoja kutoka kabila ya 'Aqeel. Mtu huyu alimfuata Mtume huku akiwa amefungwa minyororo, akaita: Ewe Muhammad, Mtume naye akamfuata, (kukazuka majadiliano yafuatayo):
**Mtume:** Vipi, una nini wewe?
**Mateka**: Kwa nini umeniteka?
**Mtume**: Kwa sababu ya kosa la washirika wako wa kabila ya Thaqiif. Kisha Mtume akaondoka.
**Mateka** akaita: Ewe Muhammad
**Mtume** akasema: Vipi una nini?
**Mateka** akasema: Mimi nimesilimu.
**Mtume** akasema: Ungesema hivyo wakati unajiweza ungekuwa umefaulu sana, kisha akaondoka.
**Mateka** akamuita: Ewe Muhammad,
**Mtume** akamjia na kumuuliza: Una nini?
**Mateka** akajibu: Kwa hakika nina njaa, nilishe, na nina kiu ninyweshe.
**Mtume** akasema, hii ni haki yako.
Mateka huyu, baadye akawa ndio fidia ya kuachiwa huru wale watu wawili waliotekwa.
Katika hadithi hii, kuna ushahidi kwamba kula na kunywa ni haki ya mateka, haifai hata kidogo kuzichelewesha, kwa sababu, pale Mtume aliposema "*Hii ni haki yako*" alikusudia kwamba, haki yako hii unaipata sasa hivi.

## KUWAPA MAVAZI MATEKA

Imeelezwa hapo juu kwamba Mtume (juu yake rehema na amani) aliwaamrisha maswahaba wake kuwakirimu mateka na kuwafanyia wema, ni wazi kwamba, wema huu hauwezi kutimia endapo mateka wataachwa bila kuwa na nguo za kuvaa, au kuachwa na midabwada au nguo zilizochakaa. Na inajulikana kwambaUislamu hauruhusu mtu kuangalia tupu ya mtu mwingine. Kwa msingi huu, ndio maana tukasema kuwa, ni haki na wajibu wa kisheria kuwapa mavazi mateka.

## HAKI YA KUHESHIMU UTU NA HADHI YA MATEKA

Uislamu umelinda utu na hadhi ya mateka. Hili linaonekana wazi pale Uislamu ulipolinda heshima ya mwanamke mateka ambaye ataangukia kuwa ni mateka. Moja ya heshima aliyopewa mwanamke ni lile katazo la kujamiiana nae kabla hajazaa au kupata hedhi. Ushahidi wa hili ni Hadithi iliyopokewa na At-Tirmidhiy kwamba Mtume (juu yake rehema na amani) "*Ameharamisha kuwaingilia wanawake mateka, mpaka wazae vilivyomo matumboni mwao*". Na ushahidi mwingine ni Hadithi iliyopokewa na Ahmad kwamba Mtume (juu yake rehema na amani) amesema, "*Yeyote mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho, asimuingilie mateka yoyote wa kike mpaka apate hedhi moja*". Sasa endapo mtu atamuingilia kijakazi wa ghanima (ngawira) kabla mgao haujafanyika, na ikawa mtu yule aliyefanya vile ana fungu lake, hapo ni lazima kwa mtu huyo atoe mahari inayoendana na hadhi ya yule mwanamke, ambayo itaongezwa katika fungu la ghanima. Lakini mtu huyu kama alikuwa ni mzinifu tu, hapo ataadhibiwa.

Kwa maelezo zaidi, Hadithi ifuatayo iliyopokelewa na Ahmad kutoka kwa Bi Aisha, inafafanua ni kiasi gani Uislamu umesisitiza kuhusu kumheshimu mwanamke. Hadithi inaeleza kwamba, pindi walipogawanywa mateka wa Banii Mustalaq, Bi Juwayriyah bint Harith alikuwa ametekwa na Thabit bin Qais bin Shamas, au tuseme kuwa Juwayriyah aliangukia kwa binamu yake. Basi Juwayriyah akaandikishiana na binamu yake, Juwayriyah alikuwa ni mwanamke mrembo, kisha akaja Mtume (juu yake rehema na amani) na Juwayriyah alipomuona Mtume akasema, 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, Hakika mimi ni Juwayriyah bint Harith bin Dhiraar (Dhiraar ni mtu mkubwa sana kwa watu wake) na kwa hakika nimekumbwa na balaa ambalo lipo wazi kabisa mbele yako, kama itakupendeza, naomba unisaidie kuhusu makubaliano niliyoyaingia.

Mtume akamuuliza hivi unataka heri nyingine kubwa zaidi ya hiyo? Juwayriyah naye akauliza: ‘Enhe ni heri gani hiyo tena ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Mtume akajibu: Maliza mkataba wako nami nitakuoa, Juwayriyah akajibu, nimekubali ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, Mtume akasema, hakika nimeshafanya hivyo. Basi habari hii ikasambaa kwa watu kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu kamuoa Juwayriyah bint Harith, watu wakawa wanasema kabila ya Bani Mustalaq washakuwa wakwe za Mtume (juu yake rehema na amani) wakawa wanapeleka vitu walivyokuwa navyo. Bi Aisha anasema, kitendo cha Mtume kumuoa Juwayriyah kilisababisha kuachwa huru watu mia moja wa kabila ya Banii Mustalaq, Bi Aisha anaendelea kusema kuwa: ‘Sijawahi kuona mwanamke yeyote aliyebahatika kuwa na baraka tele kwa watu wake kama yule‘.

## KUHIFADHI UMOJA WA FAMILIA

Wanachuoni wa Sheria ya Kiislamu wamekubaliana kuwa haifai kuwatenganisha mateka, kati ya mama na mtoto wake mdogo, hata kama mama ataridhia kufanya hivyo. Hii ni kwa kufuata amri ya Mtume (juu yake rehema na amani) aliposema, “*Wasitenganishwe, kati ya mama na mwanaye*” ni kwa sababu ya kuepusha madhara ya wazi ambayo yatamkumba mtoto. Inajulikana kwamba mwanamke anaweza kuridhia jambo ambalo linaweza kumdhuru, kisha baadae ndio moyo wake unabadalika na kuanza kujuta.

Ila kuna baadhi ya wanazuoni wameona kuwa inafaa kuwatenganisha wawili hawa pale mtoto atakapokuwa ni mkubwa, lakini wengine wameona kuwa haifai kuwatenganisha, sawa sawa mtoto awe ameshakuwa mkubwa kisheria au bado ni mtoto mdogo. Pia wanazuoni wametofautiana kuhusu umri ambao mtoto atazingatiwa kuwa ni mkubwa, baadhi yao wameona kwamba mtoto atahesabika kuwa ni mkubwa pale atakapofikia umri wa miaka saba au nane, wakati wanazuoni wengine wameona kwamba mtoto atahesabika kuwa ni mkubwa pale atakapoweza kuvaa na kutawadha yeye mwenyewe, kwa sababu muda huu huwa hana haja tena ya kuandaliwa na mama yake.

Kuna kundi la tatu la wanazuoni limeona kuwa mtoto atahesabika kuwa ni mkubwa pale atakapobalehe, hawa wanatolea ushahidi wa hili kwamba, kuna Hadithi imepokewa na Ubada bin Swamit , kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (juu yake rehema na amani) amesema: “Wasitenganishwe, kati ya mama na mtoto wake. Pakaulizwa : Mpaka lini ? Mtume akajibu: Ni mpaka

mtoto wa kiume atakapobaleghe na mtoto wa kike atakapoingia katika siku zake za hedhi“.

Hoja hii ndiyo tunayoiunga mkono, kwa sababu hiki ni kipimo madhubuti, na ni kwa sababu, mtoto huwa anajitegemea baada ya kubaleghe. Namna hiyo hiyo haifai kuwatenganisha baba na mwanaye, wala baba na babu au bibi yake, ni kwa sababu babu huzingatiwa kuwa ni kama baba, na bibi naye huzingatiwa ni mama, kama ambavyo haifai kuwatenganisha ndugu wawili wa kiume au wa kike.

## HAKI YA MATEKA KUWASILIANA NA NDUGU NA JAMAA ZAO

Uislamu haukatazi mateka kuwasiliana na kuwajulia hali ndugu na jamaa zao. Kwani hilo ni jambo linaloendana na maadili ya Kiislamu kuhusu kumhurumia binadamu na kumtukuza pamoja na kumjali na mengineyo katika maadili na misingi iliyo bora.

Pamoja na hayo yaliyotangulia, Dola ya Kiislamu ina haki ya kuchukua hatua za kilazima ili kulinda usalama wa nchi yake wakati wa kubadilishana barua na vifurushi baina ya mateka na jamaa zao, ni kwa lengo la kuzuia chochote kile ambacho kipo ndani ya barua zao na ambacho huenda kikapelekea kusambaza siri za Dola ya Kiislamu.

# UWIANO ULIOPO KATI YA SHERIA YA KIISLAMU NA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU

Hakuna tofauti yoyote baina ya Sheria ya Kiislamu na Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu kuhusiana na kuwafanyia muamala mzuri mateka na kuheshimu utu wao.

Kwani sheria zote mbili zinasisitiza kuwafanyia mateka muamala mwema na kuwapa mahitaji yote ya maisha na kuwaruhusu kuwasiliana na ndugu zao, na kwamba haifai wao kuadhibiwa, kuuawa au kuutweza utu wao. Bali Uislamu umeenda mbali zaidi kwa kuwapatia mateka muamala ulio mzuri zaidi kuliko ule uliowekwa na Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu. Na mfano wa wazi katika hili ni ule wema alioutenda Mtume (juu yake rehema na amani) pamoja na maswahaba wake kuwatendea mateka wa Vita vya Badr, pale mateka walipopewa kipaumbele na kutangulizwa katika kila jambo kabla ya waislamu wenyewe, na mengineyo mengi ambayo Uislamu umewapa mateka.

Hivyo basi, hakuna tofauti kati ya Sheria ya Kiiislamu na Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu katika maudhui hii.

## SURA YA TATU

# ULINZI KWA WATU WALIOPOTEA NA MAITI, KATIKA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU NA SHERIA YA KIISLAMU

Mlango huu una tafiti mbili

**Tafiti ya kwanza:** Ulinzi kwa watu waliopotea na maiti, katika Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu.

**Tafiti ya pili:** Ulinzi kwa watu waliopotea na maiti, katika Sheria ya Kiislamu.

# TAFITI YA KWANZA

# ULINZI KWA WATU WALIOPOTEA NA MAITI, KATIKA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU

## 1. ULINZI KWA WALIOPOTEA

Ni wajibu wa kila upande kati ya pande za mgogoro, kufanya zoezi la kuwatafuta watu waliopotea ambao tayari nchi hasimu ilishatoa taarifa ya kupotea kwao. Hili lifanyike kwa haraka iwezekanavyo pale tu mazingira yatakaporuhusu, punde tu baada ya kuisha matendo ya kiadui.

Na ni jukumu la nchi iliyopewa taarifa kuifikishia nchi hasimu taarifa zote ilizopata kuhusiana na watu hawa waliopotea, ima moja kwa moja, au kwa njia ya Nchi Yenye Kutoa Ulinzi (The Protecting State), Wakala Mkuu wa Kutafuta Waliopotea inayofanya kazi chini ya Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu au Taasisi za Kitaifa za Red Cross au Red Crescent.

Na ikitokea kwamba taarifa hizi zimefikishwa pasi na kupitia Kwa Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu au wakala wake mkuu wa kutafuta waliopotea, basi kila pande moja ya mgogoro itatakiwa kupeleka taarifa hizo kwa Wakala Mkuu wa Kutafuta Watu Waliopotea.

## 2. ULINZI KWA MAITI

Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu imeeleza kuwa ni lazima kuheshimu miili ya watu waliokufa nje ya nchi yao kutokana na shughuli za kijeshi, kama ambavyo inapasa kuwaheshimu maiti waliopoteza Maisha yao kwa sababu ya kuvamiwa au kutekwa.

Hivyo basi, ni jukumu la kila pande ya mgogoro kuzika miili hiyo kwa heshima zote na -ikiwezekana- kwa mujibu wa dini ya kila maiti, pia, na kama

itawezekana, basi kila maiti izikwe kivyake. Kama inavyolazimu kuheshimu makaburi na kuyaweka sehemu moja kulingana na utaifa wa kila maiti, huku yakiwa na alama ambayo kwayo itawezekana kuelekeza. Kwa muktadha huu, ni lazima kwa kila pande ya mapambano kuandaa idara maalumu ya kusajili makaburi. Hili lifanyike wakati wa kuanza vita, ili iwe ni wepesi kwa baadae kuelekeza na kuhakiki maiti ya mtu fulani hata kama litakuwa wapi, na ikilazimika kuuhamisha mwili huu na kuurudisha katika nchi yake.

Inakumbushwa kuwa, haifai kabisa kuchoma maiti, isipokuwa tu kwa sababu za kiafya au kama dini ya maiti hiyo itakuwa inaruhusu kufanya hivyo. Na endapo vita vitapiganwa baharini, ni lazima kuhakikisha kwamba kila maiti moja inatupwa kivyake kama mazingira yataruhusu. Na kama maiti itahamishiwa nchi kavu basi sheria zile zilizotajwa hapo juu ndizo zitakazotumika kuzika maiti hiyo.

Na kwa vyovyote vile, ni lazima kuhakiki taarifa za mtu aliyefariki na kuandaa ripoti inayomhusu. Na kwa yule maiti mwenye utaifa wa nchi mbili ni lazima abaki na nusu moja ya utaifa wake au abakie na utaifa ule ule kama atakuwa ni raia wa nchi moja. Hili lizingatiwe katika mazingira ya vita vya baharini au nchi kavu.

Itifaki ya Kwanza ya Mwaka 1977 imesisitiza juu ya umuhimu wa kurahisisha taratibu za kurudisha mabaki ya maiti na vitu vyao nchini mwao, sambamba na kuzisaidia familia za maiti na maafisa wa vitengo rasmi vinavyohusika na kusajili vifo, waweze kufika katika makaburi ya maiti zao.

Pamoja na hayo, Itifaki hiyo pia imesisitiza juu ya umuhimu wa kulinda makaburi na kuyafanyia marekebisho ya mara kwa mara, na imeitaka nchi ambayo imezika maiti hizo kuacha kutoa mabaki ya maiti hao. Lakini nchi hiyo itaruhusiwa kufanya hivyo endapo itakuwa imeomba ruhusa kwa nchi yenye maiti zake kuzifukua maiti hizo na kutaja sehemu ambayo itazizika tena. Hii ni endapo kutakuwa na dharura hasa yenye faida kwa jamii kama vile dharura za kimatibabu au sababu za kuhakiki.

# TAFITI YA PILI

# ULINZI KWA WATU WALIOPOTEA NA MAITI, KATIKA SHERIA YA KIISLAMU

## 1. ULINZI KWA WATU WALIOPOTEA

Uislamu haukatazi hata kidogo pande mbili za mgogoro kubadilishana taarifa kuhusu watu waliopotea, kwa sababu Mtume mwenyewe (juu yake rehema na amani) alikuwa akiulizia kuhusu hatma ya wanajeshi wake baada ya Vita vya Uhudi, ili apate kujua ni nani mzima na nani kauawa au kujeruhiwa, ambapo alisimama mbele ya maiti ya baba yake mdogo Hamza, huku akiwapa maswahaba wake jukumu la kuwatafuta maswahaba walioshiriki vita vile ili pajulikane kama ni wazima au laa.

Mtume (juu yake rehema na amani) anapofanya jambo kama hili sehemu ya tukio huwa lina maana ya kubaisha jambo na kulifanya lijulikane kuwa ni sheria. Hivyo basi ni wajibu wa Kiongozi wa Kiislamu kutoa juhudi awezavyo ili kutambua hali ya kila mwanajeshi wake, hata kama ni kubadilishana taarifa na maadui zake moja kwa moja au kwa njia ya nchi ya tatu isiyoegemea upande wowote, kwani hilo halina madhara yoyote.

Kitu kibaya ni kukaa bila kufanya juhudi yoyote ya kujua hatma ya wanajeshi wake. Na kwa kuwa hasimu wa Dola ya Kiislamu atakuwa anawapa taarifa waislamu kuhusiana na wanajeshi wa Kiislamu waliopo katika nchi yake, lakini pia anawatafuta wanajeshi hao hao wa Kiislamu katika nchi yake, basi hakuna kinachoizuia nchi ya Kiislamu nayo kufanya hivyo hivyo kwa wanajeshi wa nchi hasimu, na hii inaingia katika ile kanuni ya Kufanyiana Usawa au nipe nikupe, jambo hili lina faida kwa pande zote mbili na wala halina madhara yoyote kwa upande wowote.

## 2. ULINZI KWA MAITI

Uislamu unahifadhi heshima ya maiti hata kama ni maiti wa maadui. Na miongoni mwa heshima ambazo Uislamu umempa maiti ni kwamba Mtume (juu yake rehema na amani) amekataza kukatakata maiti. Ushahidi wa hili ni Hadithi iliyopokewa na Imam Ahmad na Ibn Maajah kutoka kwa Swafwan bin ‘Asaal amesema: Mtume (juu yake rehema na amani) alitutuma kwenda vitani, akatumbia "*Nendeni kwa jina la Mwenyezi Mungu, piganeni vita na anayempinga Mwenyezi Mungu, na msiwakate kate maiti, msivunje ahadi, wala msiuwe mtoto mdogo.*"

Uislamu unakataza kukatakata maiti ya mahasimu hata kama wao wataamua kukatakata maiti za waislamu. Kwa sababu katika vita vya Uhudi waislamu sitini na nne Answaar na wengine sita Muhaajiriina waliuawa, katika hao alikuwepo Hamza baba yake mdogo Mtume (juu yake rehema na amani). Jambo la kusikitisha ni kwamba wale wasiokuwa waislamu waliyatoboa matumbo ya maiti ya waislamu, kukata dhakari zao na kuwakatakata vibaya sana. Kwa upande wao, waislamu nao walipoona vile wakahamaki na kusema, kama Mwenyezi Mungu akitusaidia tukawashinda wale maadui basi patachimbika, tutafanya maradufu ya ubaya walioufanya wao, na tutawakatakata kwa namna ambayo haijawahi kutokea wala hakuna mwarabu yeyote aliyewahi kufanya kama hivyo.

Wakati waislamu wakiyasema hayo, Mtume (juu yake rehema na amani) alikuwa amesimama mbele ya maiti ya Hamza babake mdogo huku maiti hiyo ikiwa imekatwa pua na Washirikina (wasiokuwa waislamu) ambao walikuwa wamekata dhakari yake na kutoboa tumbo lake, ambapo Hindu bint ‘Utbah (mke wa Abu Sufyani) alikata kipande cha ini la Hamza na kuanza kukitafuna ili akile, lakini kipande hiki cha ini hakijakaa tumboni mwake akakitema na kukitupa, Mtume (juu yake rehema na amani) alipomuangalia Hamza alisema: "*Naapa kwa Mwenyezi Mungu, Mungu akinipa ushindi dhidi yao nitakatakata maiti zao sabini sehemu yako (kwa kulipa kisasi)*".

Hapo Mwenyezi Mungu akashusha maandiko yafuatayo: "***Na mkilipiza basi lipizeni sawa na vile mlivyo adhibiwa. Na ikiwa mtasubiri, basi hakika hivyo ni bora zaidi kwa wanao subiri.***". (16:126)

Hapo Mtume (juu yake rehema na amani) akasema, "*basi na tusubiri*". Akawa ameacha kufanya lile alilotaka, na badala yake akatoa kafara ya kuvunja kiapo

chake kile.

Na hata viongozi wa Kiislamu waliokuja baada ya Mtume (Khulafaa Raashiduun) walifuata muongozo huu huu wa kibinadamu. Itakumbukwa kwamba Ally bin Abi Talib (Mungu amridhie) aliwaasa watu wake baada ya kuchomwa vibaya sana na Bin Maljam, akisema: 'Mpeni chakula huyo na mumnyweshe, na mfanyieni wema katika kifungo chake, kama nitabahatika kuishi basi nitakuwa na haki ya damu yangu, nikitaka nitasamehe na nikitaka nitalipiza kisasi, na kama nitafariki nanyi mkaamua kumuua, basi msimkatekate'.

Ni lazima kuheshimu maiti za mahasimu ambazo zipo katika ardhi ya waislamu, kwa sababu maiti itabaki kuwa ni binadamu tu kwa namna yoyote ile, na Uislamu umemtukuza binadamu pasi na kuangalia dini yake. Kwa ajili hiyo, ni lazima kuzika maiti za hasimu na kuhifadhi utambulisho wake binafsi ili iwe ni rahisi kutambua kaburi lake. Imam Ad-Daaraqutniy amepokea Hadithi kutoka kwa 'Umar bin Abdallaah bin Ya'ala bin Murah Ath-Thaqafiy, naye amepokea kutoka kwa baba yake amesema, nimemsikia Ya'ala bin Murah akisema: 'Mimi nilishasafiri na Mtume (juu yake rehema na amani) zaidi ya mara moja, kwa hakika, sijawahi kumuona akipita mbele ya maiti ya mtu yeyote kisha aivuke tu hivi hivi (kama hajaona kitu) bali alikuwa anaamrisha azikwe, tena wala haulizi kamwe kama ni muislamu au sio muislamu.'

Jambo hili linakubaliana kabisa na vifungu vya sheria vilivyomo katika mikataba ya Geneva kwamba, ni jukumu la kila pande ya mgogoro kuhakikisha kuwa maiti zilizopo katika ardhi yake zinazikwa. Na hakuna ushahidi wowote wa kisheria unaozuia kushirikiana na adui ili kuitambua miili ya maiti au kuihamishia kwenye nchi zao na kuzikwa. Na hili limeelezwa na wanazuoni wa sheria wa madhehebu ya Ibadhi.

# UWIANO ULIOPO KATI YA SHERIA YA KIISLAMU NA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU

Tumeona ni kwa kiasi gani Sheria ya Kiislamu imeharamisha kutoheshimu maiti wa adui, na ni wazi kabisa kwamba Uislamu umekataza kukatakata maiti, jambo ambalo linaafikiana na katazo la Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu juu ya kutoheshimu maiti za watu ambao wamekufa nje ya nchi yao, sawa sawa iwe waliuawa kwa sababu ya vita ama kwa sababu ya uvamizi wa kijeshi.

Na ukweli ni kwamba, mambo ambayo yanahusiana na kuzika maiti, kuzibeba na kuzipeleka nchi nyingine pamoja na kuwarahisishia taratibu za kufika kaburini, ndugu na maafisa wa nchi ya yule marehemu, mambo ambayo yamewekwa na Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu, hayapingani kabisa na Sheria ya Kiislamu, madamu pande zote mbili za mgogoro zinatekeleza hilo.

Kwa upande wa Uislamu, dalili na msingi mkubwa wa hili ni kwamba Mtume (juu yake rehema na amani) aliamrisha kuzika maiti na kukataza kuzikatakata. Ama kuhusiana na mambo mengine ambayo hayajaelezwa wazi wazi katika Qur’an wala Hadithi za Mtume, hayo marejeo yake ni misingi ya ujumla inayoruhusu mambo haya, na ambayo inapelekea udharura wa kuyatekeleza kwa ajili ya maslahi ya umma.

Kwa kuwa nchi za Kiislamu zimesaini mikataba ya Geneva, imekuwa ni wajibu wa kisheria kutekeleza mikataba hiyo, ni kwa sababu, misingi ya mikataba hiyo inaendana na misingi iliyowekwa na Uislamu.

## SURA YA NNE

# ULINZI KWA RAIA NA VYANZO VYA HUDUMA ZA KIJAMII KATIKA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU NA SHERIA ZA KIISLAMU

Mlango huu una tafiti mbili:

**Tafiti ya kwanza:** Ulinzi kwa raia katika sheria za kimataifa ya kibinadamu na sheria za kiislamu, na tafiti hii ina vifungu viwili.

**Kifungu cha kwanza:** Ulinzi kwa raia katika Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu

**Kifungu cha pili:** Ulinzi kwa raia katika Sheria ya Kiislamu

**Tafiti ya pili:** Ulinzi kwa vyanzo vya huduma za kijamii katika Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu na Sheria ya Kiislamu

# TAFITI YA KWANZA

# ULINZI KWA RAIA, KATIKA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU NA SHERIA YA KIISLAMU

## KIFUNGU CHA KWANZA: ULINZI KWA RAIA, KATIKA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU

Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu inazitaka pande za mgogoro kutofautisha kati ya raia wa kawaida na wapiganaji. Na neno "raia" hapa linamaanisha "wananchi wote" hivyo basi, neno hilo linawalenga raia wote wanaoishi katika miji ya nchi zinazopigana vita pamoja na raia wanaoishi katika ardhi zilizovamiwa. Hii inamaanisha kwamba, raia ni kila mtu ambaye hapigani vita. Na endapo patakuwa na mashaka juu ya hali ya mtu fulani, kwamba ni raia wa kawaida au ni mpiganaji, hapo inabidi azingatiwe kuwa ni raia wa kawaida tu. Na ulinzi unaotolewa kwa raia hawa, unawahusu pia watu wote wanaofanya kazi ya kutoa misaada, waandishi wa habari, na vyombo vya usalama wa raia.

Na raia wote wa kawaida wana haki ya kupewa ulinzi kikamilifu dhidi ya hatari zitokanazo na shughuli za kijeshi zinazolenga kushambulia au kujikinga na adui, na kwamba, ulinzi huu unatakiwa utolewe katika mji wowote ambao unafanyika shughuli hizo, ikiwemo eneo halali la nchi fulani ambalo limevamiwa na kutawaliwa na adui na kugeuka kuwa ndio sehemu ya mgogoro, iwe ni bara, baharini au angani. Ikumbukwe kwamba, haifai kabisa raia hawa wawe ni sehemu ya kushambuliwa, kama vile ambavyo inapasa kuwakinga dhidi ya mashambulizi holela ambayo hayatofautishi kati ya sehemu za kijeshi na za raia, sambamba na hayo, haifai kuelekeza mashambulizi kwenye vyanzo vya huduma za kijamii.

Ni lazima kuwaheshimu raia na kukaa nao vizuri kibinadamu pasi na kuwabagua kwa misingi ya jinsia, rangi, ukoo, itikadi za kidini, kisiasa au mielekeo mingine, au kuwabagua kwa misingi ya utaifa, kijamii, hali ya kiuchumi, kuzaliwa au hali yoyote ile yenye misingi inayofana na hiyo..

Na katika mazingira yoyote, ni lazima uheshimiwe utu na utukufu wao, pamoja na haki zao za kifamilia, itikadi zao za kidini, na utekelezaji wa ibada zao. Ada na desturi zao pia ziheshimiwe. Na kwa muda wote wa vita wanatakiwa wapate muamala mzuri wa kibinadamu. Kama vile ambavyo, haifai kufanyiwa matendo yoyote ya unyang'anyi, uporaji au ulipaji wa kisasi dhidi yao au dhidi ya mali zao.

Ni wajibu kwa nchi yoyote yenye kuvamia nchi nyingine kuwapatia raia wa nchi iliyovamiwa mahitaji yote ya lazima ya kuhifadhi maisha yao, kama vile makazi, chakula, mavazi, magodoro, dawa na vitendea kazi vya ibada.

Vile vile yapasa kuwapatia raia waliopo katika eneo linalomilikiwa na moja ya pande mbili za mgogoro, misaada ya kijamii isiyokuwa na upendeleo wala ubaguzi wowote, pia yale maeneo ambayo hayakuvamiwa ikiwa hawajapelekewa vyakula na misaada ya lazima kwa ajili ya maisha yao, kama vile malazi, mavazi, vyakula, magodoro, zana za matibabu na mahitaji mengineyo ya lazima, basi ni lazima wapelekewe mahitaji hayo ya msingi kwao.

Ni lazima pia kuwe na uangalizi mkubwa wa kiafya kwa raia wote, na kuwe na uangalizi wa namna ya kipekee, kwa majeruhi, wagonjwa, wasiojiweza, wanawake waja wazito, watoto wadogo waliozaliwa karibuni na vilema.

Sambamba na hilo, ni lazima kwa pande zenye mgogoro, kurahisisha kazi ya kuziunganisha familia zilizotenganishwa na migogoro ya kutumia silaha, ili familia hizo ziweze kurudisha upya mawasiliano yake, na ikiwezekana zikusanywe pamoja. Kama ambavyo ni lazima pia kwa kila upande uhamasishe, kwa namna ya kipekee, utekelezaji wa kazi za mashirika ya kibinadamu yanayofanya kazi ya kuunganisha familia, kwa sharti kwamba, taasisi hizo zifanye kazi zao kwa kufuata maelekezo ya kiusalama yanayotolewa na pande za mgogoro.

Ni wajibu kwa watu wote wanaokaa katika eneo ambalo liko chini ya moja ya pande za mgogoro au katika eneo ambalo limevamiwa na moja ya pande hizo

kupewa ruhusa ya kutoa habari za mambo yao binafsi kuwaendea ndugu zao, na wao pia wapokee habari za familia zao.

Sheria ya kimataifa ya binadamu inawapa ulinzi mkubwa sana wanawake na watoto wakati wa migogoro ya kivita; na hili limetiliwa msisitizo na Baraza la Uchumi na Jamii, ambalo lilipeleka ombi kwa Baraza Kuu la Umoja wa Kimataifa juu ya kuangalia uwezekano wa kutoa tangazo la ulazima wa kumpa ulinzi Mwanamke na Mtoto katika hali ya dharura au nyakati za vita. Na kwa msingi huo, Baraza Kuu la Umoja wa Kimataifa lilitoa ilani hiyo mnamo tarehe 14/Desemba/1974.

Pia Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu inatoa kinga kwa wageni wakazi wanaoishi katika moja ya pande za mgogoro, kama ambavyo inawapa wageni hawa haki ya kusafiri kutoka nchi yenye vita, punde tu baada ya kuzuka vita ama wakati vita vinaendelea. Ni lazima kuwasafirisha wageni hawa pale ruhusa hiyo itakapotolewa, tena iwe katika kipindi rafiki chenye hali ya amani, na kuwa katika afya njema na kuwepo kwa chakula.

## KIFUNGU CHA PILI: ULINZI KWA RAIA KATIKA SHERIA YA KIISLAMU

Katika Sheria ya Kiislamu, haifai kuelekeza shughuli zozote za kijeshi kwa raia, bali shughuli hizo zielekezwe kwa watu wenye uwezo wa kupigana ambao wamepewa jukumu hilo. Hii ni kumaanisha kwamba, raia wa kawaida ambao hawakupewa jukumu hilo la kupigana na hawakujiingiza kwenye mapigano au kuwa ni wasimamizi na wapangaji wa mapigano hayo hawatazingatiwa kuwa ni wapiganaji. Hivyo basi, haifai kupambana nao. Na jopo la wanazuoni wa Sheria za kiislamu wanaona kwamba haifai kupambana na yeyote asiyekuwa mpiganaji. Kwa ushahidi kwamba Mwenyezi Mungu mtukufu amesema: "***Na piganeni katika Njia ya Mwenyezi Mungu na wale wanao kupigeni, wala msianze uadui. Kwani Mwenyezi Mungu hawapendi waanzao uadui." (2:190)***

Kwa upande wake, Mtume Muhammad (juu yake rehema na amani) amekataza kuua wanawake, watoto na watu wa dini waliojitenga na watu pamoja na wazee. Na kuna maandiko mengi sana juu ya hilo, ikiwemo Hadithi iliyopokewa na Imam Ahmad, Muslim, Ibn Maajah na At-Tirmidhiy, kutoka kwa Sulayman bin Buraydah, yeye amepokea kutoka kwa baba yake kuwa Mtume (juu yake rehema na amani) amesema : ***"...Piganeni vita katika njia ya Mwenyezi Mungu,***

*wapigeni wanaokufuru (wanaopinga), piganeni, wala msifiche mali, msitengue ahadi, wala msifanye vibaya kwa kumuua mtu na kumkatakata viungo, wala msiue mtoto.”*.

Hadithi yake Mtume (juu yake rehema na amani) ambayo imepokewa na Abu Dawoud, kutoka kwa Anas (Mungu amridhie) “*...msiue kikongwe wala mtoto mdogo...*”

Na kauli yake Mtume (juu yake rehema na amani) katika yaliyopokewa na Ibn Abass “*msiue watoto wala watu walio katika nyumba za ibada.*” na kauli yake Mtume (juu yake rehema na amani) katika yaliyopokewa na kundi la wanazuoni wa Hadithi (Al-Jama ‘a) isipokuwa An-Nasai kutoka kwa Umar (Mungu amridhie) kuwa amesema, ‘Alipatikana mwanamke aliyeuawa kwenye baadhi ya vita alivyopigana Mtume hivyo Mtume akakataza kuuawa kwa wanawake na watoto’

Ni wazi kwamba katazo la kuwaua watajwa hapo juu halikuja kwa sababu tu wameshindwa kushiriki moja kwa moja kwenye mapigano, bali ni kwa kuwa hawakushiriki kabisa katika mapigano hayo, hivyo basi ikitokea kwamba mtu yeyote ameuliwa miongoni mwa hawa basi ni kwa sababu ya kushiriki kwake katika kupambana na waislamu.

Na ikiwa haifai kuwaua wale wanaoweza kupigana vita ambao hawakushiriki katika kupambana na waislamu, basi ni wazi kabisa kwamba itakuwa haifai hata kidogo kumuua mgonjwa aliyechoshwa na maradhi endelevu kama vile mwenye kiharusi au mbaranga na mfano wake, vivyo hivyo mgonjwa wa akili na mwendawazimu, ambao hawawezi kushiriki katika vita.

Imebainika katika maelezo yaliyotangulia kwamba, haifai kuelekeza shughuli za kivita kwa raia (ambao hawashiriki vitani) na hasa hasa wanawake, watoto, watu wa dini, wazee na wagonjwa.

Pia imebainika kwamba Uislamu unasisitiza juu ya kuziunganisha familia, kwani wanazuoni wa Sheria ya Kiislamu wameonelea kwamba haifai kumtenganisha mama na mtoto wake, mzazi na mwanawe, mjukuu na babu au bibi yake, ndugu wawili wa kike au wa kiume, wala kati ya ndugu wa tumbo moja kama vile kumtenganisha baba mkubwa (au mdogo) na mtoto wa kaka yake, au mama mdogo na mtoto wa dada yake.

Kama vile ambavyo Uislamu unatoa ulinzi kwa mwanamke dhidi ya kitendo au kauli yoyote ambayo inashusha hadhi na utukufu wake, na kwamba Uislamu kwa namna ulivyo unamhurumia sana mwanamke mja mzito na mwenye kunyonyesha, awe ni Muislamu au si Muislamu. Pia Uislamu unataka raia apatiwe malazi, chakula, mavazi, na huduma ya afya.

# UWIANO ULIOPO KATI YA SHERIA YA KIISLAMU NA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU

Uislamu unaharamisha na kukataza kabisa kuua wanawake, watoto, wazee, wafanyakazi na wengineo ambao hawashiriki katika shughuli za kijeshi, kama ambavyo unalinda haki za wagonjwa, raia, majeruhi, na kwa kipekee wenye mahitaji maalumu. Pia unalinda heshima ya mwanamke na kumpa uangalizi maalum unaodhamini kulinda malezi ya watoto na kina mama. Kadhalika Uislamu unakataza kutenganisha familia, kati ya mtoto na mama yake, baba yake, ndugu yake wa kike au wa kiume, bibi yake na babu yake. Pia Uislamu unasisitiza sana juu ya kulinda haki za raia kuhusiana na chakula, afya, malazi... n.k. Na hizi ndizo haki zile zile ambazo Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu imezikubali. Hivyo basi, hakuna tofauti yoyote kati ya sheria mbili hizi.

# TAFITI YA PILI

# ULINZI KWA VYANZO VYA HUDUMA ZA KIJAMII, KATIKA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU NA SHERIA YA KIISLAMU

## 1. KULINDA VYANZO VYA HUDUMA ZA KIJAMII, KATIKA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU

Neno "vyanzo vya huduma za kijamii" linamaanisha, maeneo yote ambayo si ya kijeshi, ni maeneo yote ambayo hayana mchango wowote katika shughuli za kijeshi, na hata kama yataharibiwa au kuhodhiwa, iwe ni baadhi yake au yote, basi hakutakuwa na matokeo yoyote chanya kwa kufanya hivyo.

Na kwa kuwa Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu inalenga kulinda raia, kuwaheshimu, na kuishi nao vizuri, hivyo basi, inakataza kuwaacha na njaa kama moja ya mbinu za kivita, pasi na kuangalia kwamba mbinu hiyo ilitumika kwa lengo la kumshinikiza adui au kuwalazimisha raia kuhama miji yao. Hivyo, haifai kushambulia, kuharibu au kuhamisha vyanzo ambavyo ni vya lazima kwa maisha ya binadamu, kama vile vyakula, mazao, wanyama, ardhi ya kilimo na kuchungia wanyama, vyanzo vya maji, mashine za unyweshelezeaji na mahitaji mengine muhimu ya maisha ya binadamu yasiyokuwa hayo. Pia haifai sehemu hizi kutumika kama sehemu za mashambulizi ya vitisho.

## 2. ULINZI KWA VYANZO VYA HUDUMA, KATIKA SHERIA YA KIISLAMU

Hakika, kuharibu ardhi ya kilimo, mazao, wanyama, vyakula pamoja na mahitaji mengine ya lazima kwa binadamu, ni jambo lisilofaa kisheria kama hakuna ulazima wa kijeshi, kwa sababu kuharibu vyanzo hivi pasi na dharura,

(mathalani kuharibu vyanzo hivyo kwa lengo la kuwaaacha na njaa raia ili kuwalazimisha kuhama miji yao), kunazingatiwa kuwa ni uharibifu ardhini, na Mwenyezi Mungu amekataza kufanya uharibifu ardhini, kwani anasema ***'... wala msiasi katika nchi mkafanya uharibifu.''*** *(2 :60).*

Na ufisadi au uharibifu ni sifa mbaya ambayo Mwenyezi Mungu haipendi, na sifa hii Mwenyezi Mungu amewapa wanafiki aliposema: '***Na anapo tawala hufanya juhudi katika nchi kwa kufisidi humo na kuteketeza mimea na viumbe. Na Mwenyezi Mungu hapendi ufisadi.***' ***(2 :205)***

Hapa, Mwenyezi Mungu amemuelezea mtu mnafiki kwamba hamu yake kubwa huwa ni kufanya uharibifu ardhini na kuangamiza mashamba ambayo ndiyo sehemu ya kukua mazao na matunda, pia kuharibu kizazi. Na vyote hivi ni vitu ambavyo watu na wanyama hawawezi kuishi bila hivyo, na Mwenyezi Mungu hampendi mwenye sifa hii wala ambaye anafanya mambo haya.

Abu Bakar (Mungu amridhie) alimuusia na kumtahadharisha Yaziid bin Abi Sufyan kuhusu uharibifu, kwani imepokewa Hadithi kutoka kwa Yahya bin Said, kwamba Abu Bakar (Mungu amridhie) alituma majeshi kwenda miji ya Sham, akawa anatembea na Yazid. Yazid kwa wakati huo alikuwa ni amiri jeshi mkuu wa miji fulani hivi, Abu Bakar akamwambia Yazid, Nakuusia mambo kumi yafuatayo: 'Chonde chonde, usiue mwanamke wala mtoto au kizee kikongwe, usikate mti unaotoa matunda, usiharibu majengo, usichinje mbuzi au ngamia isipokuwa kwa ajili ya kumla tu, usichome mtende wala usiuzamishe, usifiche mali, wala usiwe muoga'.

# UWIANO ULIOPO KATI YA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU NA SHERIA YA KIISLAMU

Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu inafanana na Sheria ya Kiislamu katika kuharamisha na kukataza uharibifu wa vyanzo vya huduma za kijamii kwa lengo tu la kumkera adui au kuwashinikiza raia kuhama makazi na miji yao.

# ULINZI KWA SEHEMU ZA TAMADUNI NA IBADA, KATIKA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU

Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu imezipa umuhimu mkubwa sana sehemu za tamaduni na ibada, kwa kuzingatia kuwa sehemu hizo ni chakula cha kiroho kwa raia, na ni urithi wa kitamaduni kwa mataifa, bali ni wa watu wote duniani. Hivyo basi, kutokana na madhara yaliyowahi kutokea na kugusa sehemu hizi kama ule uharibifu uliofanywa na majeshi ya Nazi katika Vita ya Pili ya Dunia, UNESCO ililazimika kutunga rasimu ya sheria juu ya kulinda mali za tamaduni. Hivyo, mkutano wa kidiplomasia uliofanyika 'the Hague' uliipitisha sheria hiyo mnamo tarehe 14/Mei/1954.

Kwa upande wake, mkutano wa Geneva wa kidiplomasia uliokuwa ukijadili Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ulitoa wito kwa nchi ambazo hazijajiunga na mkataba huo kujiunga nao.

Na muda huo huo kikaingizwa katika Itifaki ya Kwanza, kifungu cha kulinda sehemu za tamaduni na ibada (kifungu 53), kifungu hiki, kimekataza kufanya kitendo chochote kitakachodhuru au kuharibu "sehemu za kihistoria, sanaa na sehemu za ibada, ambazo zinazingatiwa kuwa ni urithi wa kitamaduni au wa kiroho kwa mataifa" kama vile ambavyo kifungu hicho kimekataza kutumia sehemu hizi kwa lengo la kujiimarisha kwa shughuli za kivita au kuzifanya ni eneo la mashambulizi ya vitisho. Sambamba na hayo, kifungu hiki kimesisitiza juu umuhimu wa kuzingatia masharti ya Mkataba wa 'The Hugue' wa mwaka 1954, na sheria nyingine za mikataba ya kimataifa inayohusiana na maudhui hii.

## ULINZI KWA SEHEMU ZA TAMADUNI NA IBADA, KATIKA SHERIA YA KIISLAMU

Katika Sheria ya Kiislamu, haifai kufanya kitendo chochote cha kiadui dhidi ya sehemu hizi, kuzitumia katika shughuli za kivita, au kuzifanya ni sehemu ya mashambulizi ya vitisho, kwa sababu uharibifu wa sehemu hizi unazingatiwa

kuwa ni moja ya uharibifu uliokatazwa kisheria, kama ambavyo imetajwa hapo nyuma, na kama ilivyoelezwa katika wosia wa Abu Bakar "wala usiharibu majengo" hapa neno majengo linakusanya aina zote za majengo. Hivyo basi kuharibu sehemu hizi kumekatazwa kisheria.

Ikumbukwe kuwa, hata zile funguzi za kiislamu hazikuwa na uharibifu wowote, bali zilikuwa ni kuimarisha na kujenga, na dalili ya hili ni kwamba mpaka leo hii bado Misri inafurahia kuwa na sehemu zake za kumbukumbu za kifarao na Wakipti (Wakristu wa Misri) na hivi hivi ilikuwa katika kila mji ambao waliingia waislamu na Uislamu. Ni vizuri tukaashiria kwamba Abu 'Ubaidah alipoifungua Sham aliyaacha makanisa na madhabahu kama yalivyo, hakuyadhuru kwa chochote.

# UWIANO ULIOPO KATI YA SHERIA YA KIISLAMU NA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU

Sheria zote mbili hizi, zinakubaliana juu ya kutoa ulinzi kwa sehemu za ibada na tamaduni, kwa sababu hizo ni sehemu za lazima kwa ajili ya maisha ya binadamu, isitoshe, kulinda sehemu hizi pia ni kulinda masilahi ya mataifa, mali na urithi wake wa kibinadamu pamoja na tamaduni zake za kidini na kiroho, na kupuuzia misingi na urithi huu ni sawa na kufanya uharibifu ardhini, jambo ambalo Uislamu unalikataza, pia linapingana na maarifa ya kawaida ambayo ndio nguzo ya Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu. Hivyo basi, hakuna tofauti yoyote kati ya Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu na Sheria ya Kiislamu juu ya kulinda sehemu hizi.

# MLANGO WA PILI

# ULINZI KWA WAHANGA WA MIGOGORO YA NDANI YA KUTUMIA SILAHA

# UTANGULIZI NA MGAWANYO

Wakati tunatoa maelezo juu ya ulinzi ambao unatakiwa kutolewa kwa wale wahanga wa migogoro ya ndani, inatakiwa tuelezee kwanza kuhusu umuhimu wa utekelezaji wa Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu katika migogoro hiyo, na sehemu za utekelezaji wake katika sheria za kidunia na Sheria ya Kiislamu, hivyo basi, tafiti ya mlango huu itakuwa na sura mbili:

**Sura ya kwanza:** Umuhimu wa utekelezaji wa Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu katika migogoro ya ndani ya kutumia silaha na sehemu za utekelezaji wake.

**Sura ya pili:** Malengo ya kibinadamu ya kuwalinda binadamu yaliyoamuliwa kwa wahanga wa migogoro ya ndani

## SURA YA KWANZA

# MAANA YA UTEKELEZAJI WA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU KATIKA MIGOGORO YA NDANI YA KUTUMIA SILAHA NA SEHEMU YA UTEKELEZAJI WAKE

Makusudio ya Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu inayotekelezwa wakati wa migogoro ya ndani ya kutumia silaha, huwa linalenga yale yaliyotajwa katika Mada ya tatu katika vifungu shirika katika Mikataba ya Geneva ya mwaka 1949, na kifungu cha pili cha  nyongeza cha mwaka 1977.

Kipengele (1/1) cha kifungu cha pili cha nyongeza katika Mikataba ya Geneva ya mwaka 1949, kimetaja sehemu za kutekelezwa kwamba, utekelezwaji wa sheria hii unatakiwa uwe katika migogoro yote ya silaha ambayo haiingii katika kifungu cha kwanza cha nyongeza (kinachohusiana na migogoro ya kutumia silaha ya kimataifa) na kawaida migogoro hii (ya ndani) huwa inafanyika katika moja ya eneo ambalo nchi yake ni moja ya wajumbe waliotia saini sheria hii; kati ya majeshi ya serikali yake na majeshi mengine yaliyoasi, au kati ya majeshi yake na makundi mingine yanayotumia silaha na yanafanya shughuli zake chini ya uongozi maalumu uliopo katika eneo ambalo huendeleza shughuli zake za kijeshi kwa utaratibu maalumu, na kundi hili linaweza kutekeleza kifungu hiki cha itifaki, ila kipengele cha pili cha kifungu hiki hiki kinasema kwamba kifungu hiki cha nyongeza hakiingii katika hali za machafuko ya ndani, kwa mfano, vurugu na matendo ya fujo ya nadra na mengineyo yanayofanana na hayo ambayo hayaingii katika migogoro ya kutumia silaha.

Na watu wote ambao wanapatwa na madhara yatokanayo na migogoro ya ndani ya kutumia silaha, wanalindwa na kifungu cha pili cha nyongeza, kwa namna ambayo imeelezwa hapo juu (na ilivyotajwa katika kifungu cha kwanza); pasi na ubaguzi, kama ambavyo imetajwa katika migogoro ya kutumia silaha ya kimataifa.

Na masharti ya kifungu cha pili cha nyongeza yamesisitiza juu ya kwamba nchi yoyote ambayo ndani yake kuna mgogoro itabaki kuwa ni nchi Inayojitegemea, hivyo kifungu hicho kimekataza kuyageuza masharti yake kuwa ni kisingizio cha nchi nyingine kuingilia mgogoro kwa kutumia silaha au kuingilia mambo yake ya ndani au ya nje. Pia kimekataza kuyafanya masharti haya kuwa ni chambo cha kuuchezea utawala wake au majukumu yake juu ya kuzitetea taratibu zake kwa njia zote za kisheria, au kutetea umoja wa raia wa nchi na usalama wa  ardhi yake.

Na licha ya kwamba pande za mgogoro wa ndani wa kutumia silaha zinatofautiana na pande za mgogoro wa kimataifa wa kutumia silaha, isipokuwa kanuni ambazo zimetajwa katika kifungu cha pili cha ziada kuhusu

wahanga wa migogoro ya ndani ya kutumia silaha, zinafanana na zile kanuni na sheria za msingi zinazotekelezwa katika migogoro ya kimatafa ya kutumia silaha.

# MAKUSUDIO YA UTEKELEZAJI WA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU KATIKA MIGOGORO YA NDANI YA KUTUMIA SILAHA KATIKA SHERIA YA KIISLAMU

Katika Sheria ya Kiislamu, neno utekelezaji wa Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu katika migogoro ya ndani ya kutumia silaha, linamaanisha utekelezaji wa sheria zote zilizotajwa katika Qur'an Tukufu, Hadithi za Mtume au Ijtihadi, zihusianazo na kuishi nao vizuri na kuwalinda wahanga wa migogoro hiyo.

Na Sheria hizo hutekelezwa katika migogogro ya ndani ya kutumia silaha, ambayo wanazuoni wa Sheria ya Kiislamu wamekubaliana kuiita migogoro hiyo kuwa ni kuwapiga vita Wapotofu na Waliotoka katika umoja wa kiislamu (Khawaarij), nao ni 'wale watu ambao wanaompinga Imamu (Kiongozi) na wanaenda kinyume na umoja wa waislamu, huku wakiwa wamezua madhehebu yao peke yao.

Katika historia ya Kiislamu neno Khawaarij (waliotoka katika umoja wa kiislamu), japo kuwa linamaanisha Wapotofu, lakini pia huwa linamaanisha wale watu waliompinga Ally bin Abi Twalib, Kiongozi wa nne wa Kiislamu, pale alipokubali kuhukumiana na Muawiyah bin Abi Sufyan na kushuka sehemu inaiyoitwa Haruora, na hii ndio sababu Wapotofu hawa pia huitwa Harouriyah...Miongoni mwa watu hawa, wapo waliomwambia Ally wakati alipokuwa akitoa hotuba kuwa ''Hakuna hukumu yoyote ya sawa isipokuwa hukumu ya Mwenyezi Mungu tu" Ally naye akajibu, hilo ni neno la haki ila limelenga batili, akaendelea kuwaambia kuwa nyinyi (mnaonipinga mimi) mna haki tatu kwetu: "Hatutawazuia kuingia katika misikiti ya Mwenyezi Mungu ili muweze kumtaja mungu ndani yake, hatutawaanza katika vita, wala hatutawanyima Faiah (ni mali inayochukuliwa kutoka kwa wapiganaji ambao sio Waislamu) madamu mpo pamoja nasi".

Na neno Wapotofu, ni katika maneno yanayotumika sana kiistilahi ya wanasheria wa kiislamu, likimaanisha migogoro ya ndani ya kutumia silaha, ambayo kundi fulani katika jamii ya kiislamu hujitokezana kuipiga vita serikali halali (ya watu waadilifu) kwa madai kwamba wao tu ndio wenye haki ya utawala (kwa maana ya uongozi). Hapa tunafahamu kuwa, Wapotofu ni jamii ya waislamu wenye nguvu ambao humpinga kiongozi kwa kutumia tafsiri ambazo wanaamini kuwa ni sahihi, na huwa wanatumia nguvu ili kumng'oa madarakani.

Hapo huwa haiwezekani tena kwa ile serikali halali kutumia taratibu za kiusalama ambazo huenda zingetumika katika hali ya kuzuia fujo, maandamano...n.k. Kinachofanyika hapa ni kuandaa majeshi ili kuzuia hatari yao madamu washafikia nguvu hizi na wana uongozi na maeneo yao ya utawala.

# UWIANO ULIOPO KATI YA SHERIA YA KIISLAMU NA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU

Hakuna tofauti juu ya maana ya (migogoro ya ndani ya kutumia silaha) katika Fiqhi na Sheria ya Kiislamu na Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu, kwani migogoro ya ndani ya kutumia silaha huwa ni kati ya majeshi ya serikali halali na majeshi yaliyoasi au makundi mengineyo yanayotumia silaha. Hivyo basi, makundi haya ya uasi katika Sheria ya Kiislamu ndio makundi haya haya yaliyotajwa katika Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu, ijapokuwa wanasheria wa Kiislamu wanayaita makundi haya kuwa ni Makundi ya Wapotofu au waliotoka katika umoja, yaani Khawaarij, ila hiyo itabaki kuwa ni istilahi tu haileti tofauti yoyote katika matumizi, sawa sawa iwe katika namna ya mgogoro, nayo ni kwamba huo ni mgogoro wa ndani ambao dola kwa kutumia serikali yake halali inakusudia kulinda utawala, kujitegemea, na kuweka nidhamu mzuri, au kwa kuhusiana na haki za makundi yale mengine ambayo yanaipinga serikali halali.

Tofauti pekee iliyopo kati ya sheria mbili hizi ni kuhusiana na misingi thabiti ya kumlinda bianadamu. Kwani katika Sheria ya Kiislamu, misingi thabiti ya kumlinda binadamu inatokana na Qur‘an, Hadithi na Ijtihadi, ama katika Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu misingi hiyo inatokana na desturi na mikataba ya Kimataifa na taratibu zake.

# SURA YA PILI

# MALENGO YA ULINZI YA KUWALINDA WAHANGA WA MIGOGORO YA NDANI

Mlango huu unaohusiana na malengo ya kibinadamu ya kuwalinda wahanga wa migogoro ya ndani, una tafiti mbili

**Tafiti ya kwanza:** ulinzi kwa wapiganaji

**Tafiti ya pili:** ulinzi kwa raia

# TAFITI YA KWANZA

# ULINZI KWA WAPIGANAJI

Ulinzi kwa wapiganaji ni ule ule ulinzi uliotajwa kwa mateka, majeruhi, wagonjwa na waliokumbwa na majanga baharini na waliouawa. Kila kundi moja katika haya litajadiliwa katika mlango wake peke yake.

# KIFUNGU CHA KWANZA: ULINZI KWA MATEKA

## 1. ULINZI KWA MATEKA KATIKA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU

Kifungu cha pili cha nyongeza cha mwaka 1977 cha itifaki yaa Geneva ya mwaka 1949 kinachohusiana na migogoro ya ndani ya kutumia silaha, hakikutaja msamiati wa 'Mateka Japo kuwa kipengele cha tano cha kifungu hicho hicho kimetaja na kutambua haki ambazo Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu inawapa mateka.

Walioweka kifungu cha nyongeza waliwataja mateka kwa kutumia msamiati huu (watu ambao umeminywa uhuru wao), na labda nchi wanachama hawakupendelea kutumia neno 'Mateka ili kuzipa nafasi nchi ambazo zinaendelea na shughuli za kivita katika ardhi yake kuchukua hatua stahiki na za kilazima dhidi ya waasi, kama vile kuwakamata, kuwahoji na kuwapeleka mahakamani kwa mujibu wa sheria za nchi zao.

Mateka wa migogoro ya ndani wana uhuru na haki nyingi tu ambazo hazitofautiani sana na zile zilizopo katika migogoro ya kimataifa ya kutumia silaha. Kwani itifaki ya pili imetaja uhuru na haki hizi, ambazo kwa ufupi ni kwamba yapasa kuheshimu utu na utukufu wao, imani zao na namna ya utekelezaji wa ibada zao za kidini, na kwamba, katika hali zote, yapasa wafanyiwe muamala mzuri pasi na upendeleo. Yapasa kuheshimu na kuwapa

ulinzi pamoja na kuwatibu wale wote waliopata majeraha na maradhi miongoni mwao, sambamba na matibabu maalumu wanayoyahitaji, pia wapatiwe chakula na vinywaji kwa usawa kama walivyo raia wengine wa kawaida, na wapewe ruhusa ya kupokea misaada, kwa mtu mmoja mmoja na kwa makundi, kadhalika wapewe ruhusa ya kufanya ibada zao, na ruhusa ya kupokea na kutuma barua na kadi.

Izingatiwe kwamba ni lazima wanawake watenganishwe na wanaume, na wasimamizi wao pia wawe ni wanawake vile vile, lakini hili haliwahusu wale wanaume na wanawake wa familia moja, kwa sababu wao watakaa pamoja.

Na ni lazima kambi za mateka ziwe mbali na sehemu za vita, pia mateka hao waondolewe endapo vituo au kambi zao zitakumbwa na hatari zitokanazo na migogoro ya kutumia silaha, hii ni kama itawezekana kuwaondoa katika mazingira hayo na kuwaweka katika hali ya usalama. Na wakati wa kuwaacha huru watu ambao uliminywa uhuru wao, ni lazima kwa yule ambaye anayetoa maamuzi ya kuwaacha huru azingatie taratibu zote za lazima za uhakika zenye kudhamini usalama wao.

## 2. HAKI ZA MATEKA KATIKA SHERIA YA KIISLAMU

Jopo kubwa la wanazuoni wa Sheria ya Kiislamu wanaona kwamba haifai kumuua mateka wa Wapotofu, bali inatakiwa awekwe kizuizini tu kwa muda wote ambao vita inaendelea. Na haifai mateka kuuawa, kwa sababu amekuwa hana tena uwezo wa kufanya hatari yoyote, ni kwa kuwa yuko mikononi mwa serikali halali (watu waadilifu). Na ni lazima wale waliomuweka kizuizini walinde uhuru na ubinadamu wake, pia haifai kumtelekeza mateka majeruhi. Bali utukufu wa binadamu ambao umedhaminiwa na Uislamu kwa watu wote pasi na kuangalia dini au asili yao, (ongezea udugu wa kiislamu ambao unauunganisha umma kwa mahusiano ya kiroho) unamtaka Muislamu kuwapatia mateka chakula, mavazi, makazi na mahitaji mengineyo ya maisha wanayoyahitaji mateka wote wa migogoro ya ndani ya kutumia silaha, ni kwa kuzingatia kwamba pande zote za mapigano ni waislamu.

Na ikiwa Uislamu unampa mateka asiyekuwa Muislamu, uhuru na haki zake zote ambazo zimetajwa hapo juu katika migogoro ya kimataifa, basi ni lazima kwa mateka wa Wapotofu (katika migogoro ya ndani ya kutumia silaha) apate haki zake zote kama zilivyotajwa katika migogoro ya kutumia silaha ya

kimataifa. Na ikiwa Uislamu unalinda utukufu wa mateka wa kike asiyekuwa Muislamu, na umekataza kumtenganisha yeye na mtoto wake, pamoja na kuzingatia umuhimu wa kutenga sehemu za wanawake na wanaume, ni lazima pia uzingatie haki hizi kwa mateka wa kike wa kiislamu.

# UWIANO ULIOPO KATI YA SHERIA YA KIISLAMU NA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU

Ikiwa Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu katika kifungu chake cha pili cha nyongeza, hakijatumia neno Mateka kwa watu waliowekwa kizuizini na serikali halali, ili kuepuka sheria kutofuata mkondo wake dhidi ya waasi waliotiwa nguvuni. Baadhi ya wasomi wa Sheria ya Kiislamu pamoja na kuwa wametumia istilahi 'Mateka ijapokuwa Wapotofu (upande hasi wa serikali halali) ambao wanazingatiwa kuwa ni raia wa nchi ya kiislamu, ni waislamu ambao wanapata haki zile zile za mateka wa migogoro ya ndani zilizotajwa katika Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu. Bali Uislamu umesisitiza kuhifadhi damu zao na kulinda utukufu wao, na kuacha kuua majeruhi wao pamoja na kuwatilia umuhimu wagonjwa na kuwatibu majeruhi wao, pia na kuwapatia mahitaji ya maisha yao kwa sababu wao ni waislamu. Na kwa kuzingatia kwamba haki hizi zimewekwa kwa wasiokuwa waislamu basi kuwapa waislamu wenyewe ni lazima zaidi.

Hivyo basi, hakuna tofauti kati ya Sheria ya Kiislamu na Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu kuhusiana na waasi ambao si waislamu waliopinga serikali halali ya kiislamu (baada ya kutengua ahadi) kwani hukumu ya atakayetiwa nguvuni na serikali kati yao ni kwamba anatakiwa afanyiwe muamala wa kibinadamu, na apewe uhuru na haki zote ambazo Uislamu umewapa mateka wa vita wasiokuwa waislamu, kwa namna ambayo imeelezwa katika migogoro ya kimataifa ya kutumia silaha.

Hivyo basi, hakuna tofauti kati ya Sheria ya Kiislamu na Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu katika maudhui hii.

# KIFUNGU CHA PILI ULINZI KWA MAJERUHI, WAGONJWA NA WALIOPATA MAJANGA BAHARINI

## 1. ULINZI KWA MAJERUHI, WAGONJWA NA WALIOPATA MAJANGA BAHARINI, KATIKA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU

Kifungu cha pili cha nyongeza cha mwaka 1977 pamoja na kifungu cha tatu cha pamoja katika Mkataba na itifaki za Geneva ya mwaka 1949, vimetaja uhuru na haki zilizowekwa kwa majeruhi, wagonjwa na waliopatwa na majanga baharini wakati wa migogoro ya ndani ya kutumia silaha. Na masharti yaliyokuja katika vifungu hivi yanafanana sana na sheria zilizotajwa katika migogoro ya kimataifa ya kutumia silaha.

Kwani katika kifungu cha tatu cha shirika kilichopo katika itifaki za Geneva ya mwaka 1949, imeelezwa kwamba, ni lazima kwa wale wote walioshindwa kupigana vita kwa sababu ya majeraha na maradhi, wapatiwe muamala mzuri katika mazingira yote, tena pasi na ubaguzi, na kwamba, ni lazima wagonjwa na majeruhi wote wakusanywe na kupatiwa huduma.

Mlango wa tatu wa kifungu cha pili cha nyongeza cha mwaka 1977 (kuanzia kifungu cha 7 mpaka cha 12) vimeelezea kuhusu ulinzi unaotakiwa kwa majeruhi, wagonjwa na walipatwa na dhoruba baharini. Ambapo  katika mada ya saba maazimio yaliyotolewa ni kuwa ni lazima kuwaheshimu, kuwalinda na kukaa vizuri na watu hao, hata kama hawakushiriki katika migogoro ya kutumia silaha, na kwa haraka iwezekanavyo, wapatiwe huduma ya afya ya lazima pasi na ubaguzi wowote.

Kwa upande mwingine, kifungu cha nane kimehimiza juu ya ulazima wa kuwatafuta watu hawa (baada ya vita) na kuwakusanya kwa kadri mazingira yatakavyoruhusu, pia kuwalinda dhidi ya kuporwa na kunyang‘anywa mali zao, sambamba na kuwawekea uangalizi maalumu.

Vilevile kifungu cha pili cha nyongeza kimeelezea juu ya ulazima wa kuwapatia ulinzi watendaji na taasisi za kiafya na kidini, na kuvipa ulinzi vitengo na vitendea kazi vya usafirishaji matibabu, pamoja na kuheshimu alama maalumu ya Red Cross na Red Crescent ambayo haitakikani kutumiwa vibaya. Na hakuna tofauti kati ya kifungu cha pili cha nyongeza na yale yaliyotajwa katika kifungu cha kwanza cha nyongeza cha mwaka 1977 kuhusiana na migogoro ya kisilaha ya kimataifa.

## 2. ULINZI KWA MAJERUHI, WAGONJWA NA WALIOPATWA NA MAJANGA BAHARINI KATIKA SHERIA YA KIISLAMU

Kwa kuzingatia kwamba Wapotofu bado wanahesabiwa kuwa ni waislamu, hivyo uasi wao kwa rais wa nchi ya Kiislamu hauondoshi kinga na dhamana iliyowekwa na Uislamu kwa wafuasi wake, hata kama watafanya uasi kwa serikali halali, kwani inalazimika katika mazingira yoyote yale wapate huduma bora ya afya na wapewe heshima na ulinzi ambao unaendana na utukufu wa binadamu ambao umedhaminiwa na Uislamu kwa watu wote hata kwa wasiokuwa waislamu.

Na ikiwa Uislamu unatoa ulinzi kwa maadui ambao si waislamu, endapo wataugua, kujeruhiwa au kukumbwa na majanga na dhoruba baharini, basi ni jambo la lazima kwa watu hawa kupatiwa ulinzi huo huo katika migogoro ya ndani ya kutumia silaha (kati ya waasi na serikali halali). Ni lazima kuwalinda watu hawa katika hali zote, sawa sawa wawe ni wanajeshi au raia wa kawaida, waislamu au sio waislamu, (na kama si waislamu basi sawa sawa wawe wametoa jizya (tozo) au hawajatoa) pale tu watakapokuwa hawawezi tena kupigana na kubeba silaha dhidi ya serikali halali (ya watu waadilifu). Ni sharti ieleweke, kwamba watapatiwa ulinzi huu endapo wataacha kabisa kufanya kitendo chochote cha kiadui dhidi ya serikali halali (upande ambao umewatia mkononi).

Miongoni mwa matendo ya kiadui ni pamoja na kupangilia mwenendo wa vita. Ijulikane kwamba vita ni hali ya dharura, na kawaida dharura hukisiwa ufumbuzi wake kwa kiasi ilivyo dharura yenyewe, hivyo basi, ikishatoweka hatari ya hawa Wapotofu, hali ya dharura nayo huwa imeisha, (na kwa kuwa wameshatiwa nguvuni, hapo hatari yao huwa imeshaisha) na ndipo inapolazimika watu hawa walindwe na wasitelekezwe, na hasa ukizingatia

kwamba kuwalinda wahanga hawa ni kati ya maadili ya kibinadamu ambayo yamesisitizwa na Uislamu, kama vile Uislamu ulivyosisitiza juu ya utukufu wa mwanadamu, huruma na kuishi nae kwa upole, uadilifu..nk.

Kimsingi ni kwamba, Uislamu unakataza kumtesa mtu yeyote yule. Na kumuacha majeruhi na wagonjwa pasi na dawa au pasi na huduma ya afya, ni namna fulani ya kuwatesa, ni kutokana na yale machungu wanayoyapata kwa sababu ya magonjwa na majeraha yao. Abu 'Ubaidah amepokea Hadithi kutoka kwa Hisham bin Hakim bin Hizaam, akisema kwamba, amemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (juu yake rehema na amani) akisema: '***Hakika Mwenyezi Mungu atawaadhibu siku ya Qiyama wale ambao wanawatesa watu duniani***.

Na kwa kuwa Uislamu umekataza kwa ujumla kumtesa binadamu, hivyo ni lazima ukataze jambo hilo pia katika hali ya migogoro ya ndani ya kutumia silaha dhidi ya majeruhi, wagonjwa na waliopatwa na majanga baharini na ambao wameshindwa kuzitetea nafsi zao dhidi ya mahasimu wao; na hasa ukizingatia kwamba kuwaua, kuwatesa au kuwavunjia uutu wao hakuna faida yoyote kwa jeshi bali huhesabiwa kuwa ni moja ya aina za uharibifu na kumdhuru mtu pasi na sababu ya msingi, na jambo hili linapingana na Sheria tukufu ya kiislamu ambayo inakataza uharibifu. Kwani wagonjwa, majeruhi na waliopatwa na majanga baharini hawana tofauti na watu ambao hawashiriki katika mapigano, kama vile watoto, wanawake, watu wa dini na wazee ambao ni haramu na haifai kuwaua, kuwaadhibu au kuwavunjia uutu wao.

Ongezea katika hayo yaliyotangulia, Hadithi iliyopokelewa na Nafi kutoka kwa Abdullah bin 'Umar, kwamba mtume wa Mwenyezi Mungu, (juu yake rehema na amani) alimwambia Abdullah bin Masoud: "***Hivi unajua ni nini hukumu ya aliyepotoka katika umma huu***? Bin Masoud akasema: Mwenyezi Mungu na Mtume wake ndio wanaojua zaidi, Mtume (juu yake rehema na amani) akasema, '***Wala hawauwi majeruhi wao***.

Katika dalili zinazosisitiza kwamba haifai kuua majeruhi na wagonjwa pale wanapojizuia kufanya matendo ya kiuadui, ni ule msimamo aliochukua mtume (juu yake rehema na amani) kwa watu wa Makkah siku ile alipoifungua Makkah, ambapo hakumfanyia ubaya mtu yeyote kati yao wala hakuharibu mali zao, na ndipo mtangazaji wake aliponadi: Jamani eeeh, chonde chonde, majeruhi wasiuliwe, mwenye kukimbia asifuatwe, mateka asiuliwe, na mwenye kufunga mlango wake huyo amesalimika. Na hukumu hii ni kwa vita vyote, vya ndani na vya kimataifa. Na hakika Ally (Mungu amridhie) alisema siku ya

mgogoro wa Jamal, katika Hadithi iliyopokelewa na Al-Bayhaqiy: '(Mkipigana vita) 'Mkawashinda maadui zenu, basi msimfuate mwenye kukimbia, wala msiuwe majeruhi, na tafuteni zile ala zilizoletwa na vita, hizo zichukueni, na mali zozote zisizokuwa hizo ziacheni kwa warithi wake'.

# UWIANO ULIOPO KATI YA SHERIA YA KIISLAMU NA YA KIMATAIFA

Hakuna tofauti kati ya Sheria ya Kiislamu na Sheria ya kimataifa ya kibinadamu kuhusiana na kuwapa ulinzi majeruhi, wagonjwa na waliopatwa na majanga baharini, kwani sheria zote mbili zinawataka wafuasi wake kuwaheshimu na kukaa vizuri na wahanga hawa, sawasawa iwe walishiriki katika mgogoro wa kutumia silaha au hawakushiriki, madamu hatari yao imeshatoweka na wameacha matendo ya kiadui.

Sheria zote mbili zinawataka wafuasi wake kutoa huduma za kiafya za lazima, pamoja na kuwatafuta na kuwakusanya pamoja wahanga hawa baada ya kuisha kwa makabiliano yoyote, na kuwahamishia sehemu ambazo ziko mbali na hatari za shughuli za kijeshi.

Uislamu hautofautiani na Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu kuhusiana na maamuzi yake ya kulinda vitengo vya tiba na vifaa vya kuhamishia matibabu na mahitaji mengine ya lazima kwa kuwahudumia majeruhi, wagonjwa na waliopatwa na majanga baharini, kwani ni wajibu wa kisheria watu hawa kupatiwa huduma za afya, na wajibu huu hautimii isipokuwa kwa kuwalinda wahudumu wa vitengo vya kiafya pamoja na vitendea kazi vya kuhamishia matibabu, na kwa ajili hiyo, ndiyo maana imelazimika moja kwa moja kulinda watu na vitu vilivyotajwa hapo juu, kwa sababu (kama wanavyosema wanazuoni wa-Usuulil Fiqh) 'Ni wajibu kufanya jambo ambalo ni lazima lifanyike ili wajibu ukamilike.

Kwa ajili hiyo, imebainika kwamba hakuna tofauti kati ya Sheria ya Kiislamu na Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu katika kadhia hii.

# KIFUNGU CHA TATU KUWALINDA MAITI NA WATU WALIOKOSEKANA

## 1. ULINZI KWA MAITI NA WATU WALIOPOTEA KATIKA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU

Licha ya umuhimu mkubwa ulioelezwa katika kifungu cha kwanza cha nyongeza kuhusiana na kutoa ulinzi kwa maiti na watu waliopotea katika migogoro ya kimataifa ya kutumia silaha, kwamba imetenga kipengele cha tatu cha mlango wa pili (vifungu 32-34) cha kuwalinda hawa, licha ya umuhimu huo, kifungu cha pili cha nyongeza hakijatilia umuhimu mkubwa kwa maiti na waliokosekana katika vita vya kutumia silaha vya kimataifa, kwani hao wamejadiliwa katika kifungu cha nane kwa kifupi sana, kifungu hicho kimeeleza mwishoni kabisa kwamba '...Na kuzitafuta maiti na kutovunja heshima zao na kutoa heshima za mwisho kwa njia iliyo bora.

Maelezo haya mafupi yaliyopo katika kifungu cha pili, hayamaanishi kwamba Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu imepuuzia kuwapa ulinzi wahanga wa migogoro ya ndani ya kutumia silaha, bali inawezekana kwamba ufupilizo huu umekuja katika muundo huu, kwa kuwa kazi ya kuwatafuta, kuwazika na kuhamisha mabaki... nk, huwa haizui mizozo ya ndani ya kutumia silaha kama ile inayozuka katika migogoro ya kutumia silaha ya kimataifa, kwa sababu migogoro ya kutumia silaha ya ndani huwa inafanyika ndani ya nchi moja, hivyo ule ukaribu wa eneo la migogoro huwa unarahisisha zoezi la kupata makaburi ya ndugu na jamaa waliopoteza uhai wao, na mara nyingi zile pande zenye migogoro huwa zina mahusiano, ima ya kihistoria, kidini, kijamii au kitamaduni ambayo husaidia kutatua matatizo yanayohusiana na maiti za mgogoro wa ndani wa kutumia silaha kwa njia nyepesi na haraka zaidi.

Kwa vyovyote vile, maandiko yaliyokuja katika kifungu cha nane cha nyongeza, licha ya kuwa kimekuja kwa ufupi, ila kimetoa haki zote zilizowekwa kwa maiti katika migogoro ya ndani ya kutumia silaha, kwa namna ambayo haitofautiani sana na zile haki zilizowekwa kwa maiti wa migogoro ya kimataifa ya kutumia silaha. Hivyo basi, sheria na masharti yale yale tuliyoyataja katika mlango wa

kwanza kuhusu maiti za migogoro ya kimataifa ya kutumia silaha zinaingia pia hapa.

Ili kuweka ulinganishi au uwiano, tunaweza kusema kwamba, kama ambavyo yanavyotekelezwa masharti na sheria za kifungu cha nyongeza cha kwanza kuhusiana na migogoro ya kimataifa ya kutumia silaha, masharti ambayo yanahusu waliopotea katika vita vya ndani vya kutumia silaha, namna hiyo hiyo, masharti yaliyokuja katika mlango wa kwanza kuhusiana na migogoro ya kimataifa ya kutumia silaha yanatakiwa kutekelezwa. Ni kwa sababu kifungu cha pili cha nyongeza hakijaeleza wazi ulinzi uliowekwa kwa watu hawa, isipokuwa yale yaliyotajwa katika kifungu cha nne kinachohusiana na haki za msingi zinazotolewa kwa wahanga wa migogoro ya kutumia silaha ya ndani, katika kipengele cha tatu (B) ambapo maelezo yake yametaja ulazima wa '*Kuchukua hatua zote zinazostahiki ili kuwepesisha kuzikutanisha familia ambazo zilitenganishwa kwa kipindi fulani, kwa sababu ya migogoro ya ndani ya vita vya kutumia silaha.*

Na katika mambo yasiyokuwa na shaka ni kwamba upande wa mgogoro una wajibu wa kukusanya familia zilizosambaratika, katika migogoro ya ndani ya kutumia silaha na kutafuta waliopotea (wa upande mwingine) katika mji ambao una utawala, na kutoa taarifa ya majina na maelezo yao, haya yatimie kwa kushirikiana na upande wa pili kwa namna ambayo imetajwa hapo juu katika migogoro ya kimataifa ya kutumia silaha. Kwani muamala wa kibinadamu uliotajwa katika Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu unazitaka pande mbili za migogoro kushirikiana katika kutafuta watu waliopotea katika mgogoro huo na kupeana maelezo yanayowahusu watu hao.

## 2. KUTOA ULINZI KWA MAITI NA KUWATAFUTA WATU WALIOPOTEA, KATIKA SHERIA YA KIISLAMU

Jopo kubwa la wanazuoni wa sheria za kiislamu wanaona kwamba maiti za Wapotofu (waasi wa serikali ya kiislamu) inatakiwa zioshwe, zikafiniwe (kuvishwa sanda), ziswaliwe na kuzikwa, na kwamba maiti hizo zinazo haki na dhamana zote ambazo zimewekwa na Uislamu kwa maiti za waislamu nayo ni kufuata maelezo ya Mtume (juu yake rehema na amani) yaliyokuja katika hadithi iliyopokelewa na Abu Hurayrah kwamba "*na swala ni lazima kwa kila Muislamu, awe mwema au muovu na hata kama atatenda dhambi kubwa kiasi gani*

Ama kwa maiti ambazo si za Waislamu zilizopatikana katika migogoro ya ndani ya kutumia silaha, basi nazo pia zina kinga ile ile iliyotajwa katika maiti za migogoro ya kimataifa ya kutumia silaha.

Na Sheria zile zile zinazohusiana na watu waliopotea katika migogoro ya kimataifa ya kutumia silaha zinatumika pia kwa waliokosekana katika migogoro ya ndani ya kutumia silaha, kwa sababu huu ndio muamala wa kibinadamu uliowekwa na Uislamu kwa wahanga wa migogoro ya kutumia silaha iwe ya kimataifa au ya ndani.

# UWIANO ULIOPO KATI YA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU NA SHERIA YA KIISLAMU

Hakuna tofauti kati ya Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu na Sheria ya Kiislamu kuhusiana na kutoa ulinzi kwa maiti na watu waliopotea, ni kwamba sheria zote mbili zinakubaliana kwamba maiti inatakiwa ziheshimiwe na zizikwe kwa namna inayolinda utukufu wao, na kuwarahisishia ndugu wa maiti kufika katika makaburi ya ndugu zao, na kuwafanyia wepesi taratibu za kuhamisha mabaki ya maiti ya ndugu zao yafike kwenye miji yao na kwenye makaburi maalumu yaliotengewa katika mji huo, na kwamba haifai maiti kukatwa vipande vipande. Kama ambavyo sheria mbili hizi, zinavyowiana kuhusiana na ulazima wa kushirikiana katika kutafuta waliopotea katika mgogoro na kupeana maelezo juu yao.

# TAFITI YA PILI

# ULINZI KWA RAIA

## 1. ULINZI KWA RAIA, KATIKA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU

Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu imesisitiza sana juu kuwalinda raia waliopo katika mgogoro wa ndani wa kutumia silaha, kwani mlango wa nne wa kifungu cha pili cha nyongeza cha mwaka 1977 kimethibitisha ulinzi huu. Ambapo kifungu cha 13 kinaeleza kwamba raia wote wa kawaida wana haki ya kulindwa kikamilifu dhidi ya hatari zitokanazo na shughuli za kijeshi.

Ili ulinzi huu utekelezwe kwa namna iliyo bora zaidi, haifai kabisa raia kushambuliwa kwa namna yoyote ile, kama ambavyo haifai kufanya matendo yoyote ya kutumia nguvu au vitisho ambavyo vitawapa hofu raia. Na raia hawa watabaki katika ulinzi huu kwa muda wote ambao hawatashiriki moja kwa moja katika shughuli za kiadui.

Vile vile kifungu cha pili cha nyongeza kimekataza kuwalazimisha raia watoke katika ardhi yao au kuwaamrisha kuhama, lakini wanaweza kuondolewa pale tu itakapotokea dharura hasa ya kijeshi, au kwa lengo la kuwapatia usalama. Kifungu hicho hicho kimesisitiza pia juu ya umuhimu wa kuweka ulinzi katika vyanzo vya dharura vya kuwalinda raia, kama ambavyo imekataza kuwaacha na njaa raia kama moja ya mbinu za kivita. Pia kimeamrisha kuweka ulinzi sehemu ambazo zina mitambo ya kiufundi na viwanda vyenye nishati hatari, sanjari na kulinda sehemu za tamaduni na ibada; na ya kwamba haifai kushambulia maeneo haya au kuyabomoa na kuyaharibu.

Kipengele cha 18 cha kifungu hicho hicho cha nyongeza kimeweka masharti maalumu ya kuzipa ulinzi taasisi za misaada; kwamba inafaa kwa taasisi hizi kuendesha huduma zake za kimisaada katika eneo la upande uliotia saini (kama vile taasisi za Mwezi Mwekundu na Msalaba mwekundu na Simba na Jua lekundu) huduma ambazo kawaida hutolewa wakati wa migogoro ya kutumia silaha, kama ambavyo kimeeleza kwamba inafaa kwa raia wa kawaida kufanya

kazi ya kukusanya majeruhi, wagonjwa na waliopata majanga baharini, na kuwapatia huduma na mahitaji yao. Na inatakiwa kutoa huduma za kimisaada ya kibinadamu pasi na ubaguzi wowote, kwa sharti kwamba upande uliotia saini uwafiki juu ya hilo.

Kiuhalisia, takriban masharti haya ndiyo yale yale yaliyowekwa kwa ajili ya kuwalinda raia wa migogoro ya kutumia silaha ya kimataifa, kwa sababu huo ndio muktadha wa muamala mzuri wa kibinadamu uliotajwa hapo nyuma.

## 2. ULINZI KWA RAIA, KATIKA SHERIA YA KIISLAMU

Ikiwa Sheria ya Kiislamu inawapa ulinzi raia wasiokuwa waislamu katika migogoro ya kutumia silaha ya kimataifa, endapo tu watakuwa hawakushiriki katika kupambana na waislamu, wala hawakuwafanyia matendo yoyote ya kiadui, kwa namna ambayo imetajwa hapo nyuma katika migogoro ya kutumia silaha ya kimataifa, kama vile kuwalinda wanawake, watoto, wazee, vilema, watu wa dini, wafanyakazi, wakulima na rai wengineo ambao hawashiriki katika matendo ya kiadui, ikiwa Uislamu umewalinda watu hao, basi ni lazima pia uwalinde raia waliopo katika mgogoro wa ndani wa kutumia silaha, ambao hawashiriki katika matendo ya kiadui, na lazima pia uwapatiwe ulinzi ule ule uliotajwa kwa kirefu hapo nyuma katika migogoro ya kimataifa ya kutumia silaha, kama ambavyo ni lazima kwa pande za migogoro ya ndani kulinda sehemu na vyanzo vya lazima kwa maisha ya raia.

# UWIANO ULIPO KATI YA SHERIA YA KIMATAIFA YA KIBINADAMU NA SHERIA YA KIISLAMU

Hakuna tofauti yoyote kati ya Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu na Sheria ya Kiislamu kuhusiana na kuwapa ulinzi raia na vyanzo vya lazima vya maisha, kwani sheria zote mbili zinawapa ulinzi wahanga wa migogoro ya ndani ya kutumia silaha dhidi ya mashambulizi au kuwalazimisha kuhama makazi yao, kama ambavyo zinazuia kuwafanyia chochote ambacho hakina ulazima kwa shughuli za kijeshi.

Kana kwamba mfanano huu upo pia katika mgogoro wa kimataifa wa kutumia silaha, kwa namna ambayo imeelezwa hapo juu.

# MWISHO WA TAFITI

Katika tafiti yetu hii inayohusu kuwapa ulinzi wahanga wa migogoro ya kimataifa na isiyo ya kimataifa ya kutumia silaha, yenye lengo la kuweka ulinganishi au mfanano kati ya Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu na Sheria ya Kiislamu, tunaweza kupata matokeo yafuatayo:

**Kwanza:** Neno Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu ni msamiati mpya, ukilinganishwa na kanuni pamoja na Sheria za Kiislamu ambazo zimewapa wahanga wa vita kinga na haki za binadamu wakati wa migogoro ya kimataifa ya kutumia silaha, tangu zaidi ya miaka 1400 iliyopita.

**Pili:** Walengwa wa msamiati (Wahanga wa migogoro ya kimataifa ya kutumia silaha) ni majeruhi, wagonjwa, mateka, waliopatwa na majanga baharini na watu waliopotea, ambao hawashiriki katika shughuli za kijeshi. Wanaingia katika orodha hii pia kila raia wa kawaida ambao wanawahudumia wanajeshi, kama vile taasisi za kidini, kimatibabu, waandishi wa habari wa kivita, sambamba na raia wengine wa kawaida, kama vile wanawake, watoto, wazee, wafanyakazi na makundi yote ambayo hayashiriki katika vita. Na ili kuwalinda raia, yapasa sehemu za huduma za lazima kwa wananchi kwa ajili ya maisha yao nazo zilindwe, pamoja na sehemu zao za kiroho na tamaduni......n.k.

**Tatu:** Ikiwa Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu inawaangalia wahanga wa vita kwa mtazamo wa kibinadamu, kwamba wanatakiwa kulindwa wao, haki na uhuru wao, kwa sababu uwepo wao hausababishi hatari yoyote dhidi ya mahasimu wao, na ikiwa kuwapokonya haki na uhuru wahanga hawa ni kuvuka dharura za kijeshi, basi Sheria za Kiislamu nazo pia zinawaangalia hawa kwa mtazamo huo huo na zinawapa kinga hiyo hiyo. Hivyo basi, hakuna tofauti yoyote kati ya sheria mbili hizi katika hili.

**Nne:** Maandiko ya Sheria za Kiislamu (Qur'an na Hadithi) na Ijtihadi (mitazamo na utafiti) ya wanazuoni wa Sheria ya Kiislamu inawapa ulinzi sawasawa wahanga wote wa migogoro ya kutumia silaha ya kimataifa na ya ndani. Na kwa hakika, wahanga wa migogoro hii wamepata ulinzi huu tangu kuanza kwa Uislamu, kama ambavyo Mtume wa Mwenyezi Mungu na viongozi waliokuja baada yake wamesisitiza sana juu ya umuhimu mkubwa wa kuwalinda

wahanga wa vita, pasi na kuangalia dini, utaifa au ukoo....nk. na kama ikitokea kwamba kuna watu wamekwenda kinyume na sheria za kiislamu, basi Uislamu usibebeshwe lawama kwa hilo, badala yake, wabebeshwe waislamu wenyewe, iwe ni viongozi au raia ambao wamevunja haki na uhuru wa wahanga wa migogoro ya kutumia silaha, haki ambazo zimewekwa na Uislamu, tena kwa namna ambayo ni zaidi ya ilivyo katika Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu katika zama za sasa.

**Tano:** Kanuni za Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu zimepata kinga kubwa sana katika sheria za kiislamu, ambazo waislamu wanatakiwa kuzitekeleza, kwa kuzingatia kwamba ni sheria zilizowekwa na Mwenyezi Mungu mtukufu, hivyo mwenye kukiuka sheria hiyo ataadhibiwa mara mbili, ya kwanza ni hapa hapa duniani, chini ya kiongozi (rais, kamanda mkuu wa jeshi...nk.) na ya pili ni siku ya Kiama. Na hii inamfanya mpiganaji wa kiislamu, mwananchi au kiongozi ashikamane na mafundisho ya kiislamu katika jambo hili. Kwa kuwa endapo mpiganaji wa kiislamu ataweza kukimbia adhabu ya duniani, basi hataweza kukimbia adhabu ya siku ya Kiama.

**Sita:** Haki zilizowekwa kwa wahanga wa migogoro ya ndani ya kutumia silaha, takriban ni sawa na haki zilizowekwa kwa wahanga wa migogoro ya kimataifa ya kutumia silaha. Na Jumuiya za Kimataifa zimeenda mbali zaidi ziliposaini kifungu cha pili cha nyongeza cha mwaka 1977, kilichoambatanishwa katika itifaki na mikataba ya Geneva ya mwaka 1949, hasa ukizingatia kwamba hivi sasa dunia nzima inasikitishwa na hali ya wahanga wa migogoro ya kutumia silaha katika nchi za Afghanistan, Somalia, Yugoslavia (iliyosambaratika) na Dagestan..nk. hii inapelekea kwamba, ni lazima kuwe na sheria ambazo yapasa zitekelezwe na pande za migogoro ili kuwalinda wahanga wa migogoro ya ndani.

**Saba:** Ikiwa Jumuiya za kimataifa zimeenda mbali zaidi kwa kuunda Mahakama za makosa ya jinai ili kuwahukumu washtakiwa wa makosa ya kivita, kama ilivyotokea katika kesi za Nuremberg na Tokyo, na kama inavyoendelea hivi sasa katika Mahakama kuu ya Kimataifa ya makosa ya jinai, kwenye mashauri ya washtakiwa wa makosa ya vita vya Yugoslavia, vivyo hivyo yapasa kuanzisha Mahakama ya Kimataifa ya Makosa ya Jinai (itakayosimamiwa na Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu) ambayo itakuwa na nguvu ya kutuhumu, kupeleleza na kutoa hukumu, ili utekelezaji wa Sheria ya Kimataifa ya Kibinadamu uweze kufanyika katika njia iliyo bora zaidi.

Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu huwasaidia waathirika wa vita na vurugu zingine, ikifanya kila iwezavyo ili kulinda hadhi yao na kupunguza mateso wanayopitia, ikishirikiana na washiriki wake wa Red Cross na Red Crescent. Shirika hili pia hujaribu kuzuia taabu kwa kueneza na kukuza sheria za kibinadamu za kimataifa na kutetea kanuni za kimataifa za kibinadamu.

Watu wanafahamu kwamba wanaweza kuitegemea Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu kutoa huduma za kuokoa maisha katika maeneo ya vita na kufanya kazi kwa kushirikiana na jamii zilizoko huko, ili kuelewa na kushughulikia mahitaji yao. Inatambulika kwamba, uzoefu na utaalamu wa Shirika hili umelifanya liweze kukidhi mahitaji kwa haraka, tena kwa ufanisi na bila kuegemea upande wowote.

International Committee of the Red Cross
Nairobi Regional Delegation,
Denis Pritt Road
P. O. Box 73226-00200 Nairobi, Kenya
T +254 20 272 3963
E-mail: nairobi@icrc.org

International Committee of the Red Cross
Hamza Aziz Street,
Plot No1736, Block B, Kahama Court-Masaki,
P.O. Box 23431 Dar es Salaam, Tanzania
T: (+255) 222 600 446/7/8/9
E-mail : daressalaam@icrc.org
www.icrc.org
© ICRC, December 2019

0026/400 12.2019 200